epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 5, 2025 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com 0677 020 710

ISSN 0856 • No. 0581913

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 4

**Bil.** 260/- za CSR Bwawa la Nyerere zasuasua miaka minne bila uamuzi

UKURASA WA 7

**Mkutano** wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati waiva



UKURASA WA 17

**Trump** kusomewa hukumu kabla ya kuingia Ikulu



**Cheongsam zaidi ya vazi**

UKURASA 13

## MATOKEO LA NNE, KIDATO CHA PILI:

# Udanganyifu bado tatizo

UKURASA 2



151 wafutiwa matokeo



majibu yafichwa msalani




Kiingereza mfupa mgumu shule za msingi, hisabati...



Kituo chafungiwa, kigogo NECTA asema shule ifutwe



Walimu kufutwa kazi kwa kuhujumu mitihani ya taifa



Wanaoandika matusi nao bado wapo nchini



102,368 wakacha mtihani la nne, 72,179 wa kidato cha pili

# Trafiki wasimamisha na kukagua gari la waziri, mwenyewe alonga

UKURASA 5

MAISHA YALIVYO

## Mwanamume usikubali katu kulishwa na mwanamke

UKURASA 11

**MICHEZO** GUSA, ACHIA YAIVURUGA MAZEMBE UK.24

**MAONI,** UK.6

MATOKEO LA NNE, KIDATO CHA PILI

# Udanganyifu bado tatizo

Na Waandishi Wetu

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetangaza matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili Mwaka 2024, likieleza kuwa changamoto ya udanganyifu bado ipo katika baadhi ya vituo.

Kutokana na dosari hiyo, NECTA imekifungia kituo S2527 cha Shule ya Sekondari Good-Will mkoani Arusha kuwa Kituo cha Upimaji wa Mitihani ya Taifa kutokana na ilichoeleza kuwa "Mkuu wa Shule na baadhi ya walimu kudhibitisha kufanya udanganyifu kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wao".

Katibu Mtendaji NECTA, Dk. Said Mohamed, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akitangaza matokeo ya upimaji huo uliofanyika mwezi Oktoba na Novemba mwaka jana.

Alisema kituo hicho kinafungiwa kwa mujibu wa Kifungu 4(8) cha Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016 hadi hapo baraza litakapojiridhisha kuwa ni salama kwa uendeshaji Upimaji wa Mitihani ya Taifa.

"Kituo hiki kilijaribu kuwarubuni wasimamizi na askari polisi Oktoba 28, 2024, ikashindikana. Mkuu wa Shule hiyo akajaribu tena kuwarubuni wasimamizi wetu Oktoba 29, 2024, ikashindikana tena.

"Hivyo, wakaamua kutumia mbinu mbadala ya kuandaa majibu kwa kuhusisha walimu wa shule hiyo wakati mtihani unaendelea na kuwapanga wanafunzi kupata majibu... (alitaja neno lenye maana ya msalani).

Dk. Mohamed alisema pamoja na kituo hicho kufungiwa, baraza litawasilisha pendekezo rasmi kwa Kamishna wa Elimu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kufutiwa usajili wake moja kwa moja.

"Kituo hiki si tu kinakosa sifa ya kuwa kituo cha mtihani, bali kinakosa sifa ya kuendelea kuwa shule. Bila shaka mzazi anapopeleka mtoto shuleni, anatarajia pamoja na elimu, apate malezi bora na maadili na si kufundishwa udanganyifu," alisema.

Katibu Mtendaji alisema bila juhudi za ziada kudhibiti jaribio hilo, wangetangaza kufuta matokeo yote ya wanafunzi wa Kidato cha Pili shuleni huko.

"Kufutiwa kituo hicho maana yake baraza halitopeleka mtihani hapo kuanzia mwaka 2025. Wito kwa wazazi, wafikirie endapo hapo ni mahali salama kwa watoto wao kuendelea kupata elimu ya sekondari," alisema.

Kuhusu hatua kwa walimu waliowezesha utoro kwa wanafunzi na kisha kufanyiwa mtihani katika mikoa ya Mwanza na Songwe, Dk. Mohamed alisema wamefungiwa kushiriki kazi zote za Baraza la Mitihani katika kipindi chote.

Alisema pamoja na hatua zilizochukuliwa na Kamati za Mikoa, baraza litawasilisha hoja kwa mamlaka zao za ajira ili kuchukuliwa hatua za kinidhamu za utumishi wa umma, ikiwamo kutenguliwa madaraka ya ukuu wa shule, kufutwa kazi serikalini na kufunguliwa mashtaka ya jinai ya kuhujumu mitihani ya taifa.

Hata hivyo, Dk. Mohamed alisema takwimu za udanganyifu zinaonesha kupungua mfululizo kwa miaka ya karibuni.

Alisema baraza haliwezi kuwavumilia wale wanaopanga kuhujumu elimu kwa kuwa hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

### MATOKEO YALIYOFUTWA

Katibu Mtendaji alisema katika Mtihani wa Upimaji wa Taifa wa Darasa la Nne, baraza limefuta matokeo yote ya wanafunzi 100 waliofanya udanganyifu na watano walioandika matusi kwenye skripti zao.

"Wapo wanafunzi wawili walifanya udanganyifu kwa kusaidiana ndani ya chumba cha mtihani. Wanafunzi 98 ni watoro wa muda mrefu shuleni, hivyo walimu wakuu waliwapanga wanafunzi wenzao wa darasa la tano na sita kufanya mtihani kwa maslahi yao binafsi," alisema.

Pia alisema wamefuta matokeo yote ya wanafunzi 41 waliofanya udanganyifu na watano walioandika matusi kwenye skripti zao katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili.

Kuhusu wanafunzi waliofeli darasa la nne na kidato cha pili, Dk. Mohamed alisema wanapata fursa ya kukariri darasa mpaka watakapopata umahiri huo.

Katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne, alisema jumla ya wanafunzi 1,633,279 walisajiliwa kuufanya wakiwamo wasichana 839,515 sawa na asilimia 51.40 na wavulana 793,764 sawa na asilimia 48.60.

Alisema kati ya wanafunzi waliosajiliwa, 1,530,911 walifanya upimaji, wakiwamo wasichana 797,691, sawa na asilimia 95.02 na wavulana 733,220 sawa na asilimia 92.37. Wanafunzi 102,368, sawa na asilimia 6.27 hawakufanya upimaji.

Dk. Mohamed alisema Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili, jumla ya wanafunzi 879,352 walisajiliwa kufanya upimaji huo wakiwamo wasichana 476,244 sawa na asilimia 54.16 na wavulana 403, 108 sawa na asilimia 45.84.

Alisema kati yao, 879,352 waliosajiliwa, watahiniwa wa shule walikuwa 869,743 na wa kujitegemea ni 9,609.

Alisema kati ya wanafunzi 869,743 wa shule waliosajiliwa, 797,564 sawa na asilimia 91.70 walifanya upimaji ambapo wasichana ni 437,833 sawa na asilimia 93.09 na wavulana ni 359,731 sawa na asilimia 90.07. Wanafunzi 72,179 sawa na asilimia 8.30 hawakufanya upimaji.

Alisema kati ya wanafunzi 9,609 wa kujitegemea waliosajiliwa, wanafunzi 7,527 sawa na asilimia 78.33 walifanya upimaji na 2,082 sawa na asilimia 21.67 hawakufanya upimaji.

### UFAULU WA JUMLA

Dk. Mohamed alisema jumla ya wanafunzi 1,320,227 kati ya 1,530,805 wenye matokeo sawa na asilimia 86.24 wamefaulu kuendelea na Darasa la Tano mwaka 2025 kwa kupata daraja A, B, C na D.

Alisema mwaka 2023, wanafunzi waliofaulu walikuwa 1,287,934 sawa na asilimia 83.34. Hivyo kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 2.90 kwa wanafunzi waliopata fursa ya kuendelea Darasa la Tano kulinganishwa na 2023.

Alisema kuwa kati ya wanafunzi waliofaulu kuendelea, wasichana ni 699,901 sawa na asilimia 87.75 na wavulana ni 620,326 sawa na asilimia 84.61. Takwimu zinaonesha wasichana wamefaulu zaidi kulinganishwa na wavulana.

### UBORA WA UFAULU

Dk. Mohamed alisema wanafunzi wa shule waliopata Madaraja ya A-C ambayo ni ya ubora wa ufaulu ni 931,468 sawa na asimia 60.85. Mwaka 2023 walikuwa 809,379 sawa na asilimia 52.38. Hivyo ubora wa ufaulu umeongezeka kwa asilimia 8.47 kulinganishwa na mwaka 2023.

"Kuna uwiano mzuri wa ubora wa ufaulu kati ya wasichana na wavulana. Wavulana waliopata madaraja A-C ni 445,673, sawa na asimia 60.79 na wasichana ni 485,795 sawa na asilimia 60.90," alisema.

Alisema idadi ya shule katika makundi ya umahiri inaonesha kuwa kati ya shule zote 20,036, shule 12,865 sawa na asilimia 64.20 zimepata wastani wa daraja A-C, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.75 kulinganishwa na mwaka 2023.

Alisema shule 19,839 sawa na asilimia 99.01 zimepata wastani wa daraja A-C.

Dk. Mohamed alisema ufaulu wa somo la Kiswahili ni asilimia 84.52 na English Language ni asilimia 68.86 ambapo katika somo la Kiswahili umepanda kwa asilimia 0.37 na English Language umeshuka kwa asilimia 3.68 kulinganishwa na mwaka 2023.

"Ufaulu masomo ya Sayansi ya Jamii ni mzuri, masomo ya Sayansi na Hisabati ufaulu wa somo la Sayansi na Teknolojia ni asilimia 87.87 na somo la Hisabati ni asilimia 71 ambapo katika somo la Sayansi na Teknolojia umeongezeka kwa asilimia 1.01 na somo la Hisabati umeongezeka kwa asilimia 17.40 kulinganishwa na 2023.

"Wasichana wamefaulu vizuri zaidi katika somo la Sayansi na Teknolojia, lakini wavulana wamekuwa bora katika somo la Hisabati," alisema.

Kwa upande wa upimaji Kitaifa Kidato cha Pili, Dk. Mohamed alisema jumla ya wanafunzi wa shule 680,574 kati ya 796,825 wenye matokeo ambao ni sawa na asilimia 85.41 wamefaulu kuendelea Kidato cha Tatu ambapo wamepata madaraja I, II, III na IV.

"Mwaka 2023, wanafunzi waliofaulu walikuwa 592,741 sawa na asilimia 85.31. Hivyo, ufaulu umeongezeka kwa asilimia 0.10," alisema.

Alifafanua kuwa kati ya wanafunzi 680,574 walifaulu kuendelea na Kidato cha Tatu, wasichana ni 367,457 sawa na asilimia 83.99 na wavulana ni 313,117 sawa na asilimia 87.13. Hivyo, wavulana wamekuwa na ufaulu bora kuliko wasichana.

Alisema wanafunzi wa kujitegemea waliofaulu na kupata sifa ya kufanya mtihani Kidato cha Nne ni 4,205 sawa na asilimia 55.94.

### UBORA WA UFAULU

Dk. Mohamed alisema ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata wanafunzi wa shule unaonesha waliopata madaraja I- III ni 239,707 sawa na asilimia 30.08 mwaka 2023 walikuwa 192,633 sawa na asilimia 27.73. Hivyo ubora wa ufaulu umeongezeka kwa asilimia 2.35.

Katibu Mtendaji alisema ufaulu wa somo la Historia na Geografia ni wa wastani ambapo Historia ni asilimia 56.37 na Geografia ni asilimia 58.51.

"Katika somo la Civics ufaulu umeshuka kutoka asilimia 48.27 mwaka 2023 hadi asilimia 33.24 mwaka 2024. Somo la Kiswahili na Chinese Language ni mzuri sana ambapo katika somo la Kiswahili ni asilimia 91.74 na somo la Chinese Language ni asilimia 90.82.

"Masomo ya Arabic Language na French Language yana ufaulu wa wastani ambapo ufaulu wa masomo hayo ni kati ya asilimia 51.06 hadi 69.07.

"Katika somo la English Language ufaulu umeongezeka kutoka Asilimia 68.27 mwaka 2023 hadi asilimia 74.58 mwaka 2024.

"Masomo ya Sayansi Asili, Hisabati na Teknolojia, ufaulu wa masomo ya Engineering Science, Information & Computer Studies na Home Economics ni wa wastani ambao ni kati ya asilimia 51.46 hadi asilimia 62.97," alisema.

Dk. Mohamed alisema masomo ya Biology yana ufaulu ulio chini ya wastani ambao ni kati ya asilimia 18.85 hadi 47.00.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa, ufaulu wa masomo ya Home Economics, Physics, Chemistry na Additional Mathematics unazidi kuimarika ambapo kwa mwaka 2024 ufaulu umeongezeka kati ya asilimia 3.18 hadi 14.65 kulinganishwa na mwaka 2023.

Alisema katika somo la Biology ufaulu umeshuka kutoka asilimia 55.74 mwaka 2023 hadi asilimia 47.00 mwaka 2024.

Alisema ufaulu wa somo la Book-Keeping umeendelea kubaki kuwa wa wastani kwa asilimia 51.51 na ufaulu wa somo la Commerce umeshuka kutoka asilimia 50.28 mwaka 2023 hadi asilimia 43.77 mwaka 2024.

"Ufaulu waa somo la Fine Art, Theatre Arts na Music ni mzuri ambapo katika somo la Fine Art ni asilimia 84.16, Theatre Arts ni asilimia 71.35 na somo la Music ni asilimia 80.91 . Somo la Physical Education lina ufaulu wa chini ya wastani ambapo ni asilimia 25.24," alisema.

Dk. Mohamed alisema masomo yote ya ufundi yana ufaulu wa juu ya wastani ambapo somo lenye ufaulu wa juu ni Building Construction lenye ufaulu wa asilimia 84.79 likifuatiwa na somo la Electrical Engineering lenye ufaulu wa asilimia 83.66.

Alisema somo lenye ufaulu wa chini kabisa ni Woodword and Painting Engineering lenye ufaulu wa asilimia 59.20.

Alisema masomo ya dini yameonesha mabadiliko makubwa ya ufaulu, somo la Bible Knowledge limeongezeka ufaulu kutoka asimia 84.01 mwaka 2023 hadi asilimia 94.14 mwaka 2024 na somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu limeongezeka ufaulu kutoka asilimia 68.32 mwaka 2023 hadi asilimia 71.41 mwaka 2024.

HABARI KITAIFA

# Bodaboda waanza mwaka vema kwa kukabidhiwa helmet 200

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

WAENDESHA pikipiki wa kata ya Mbwara, Mkoa wa Kipolisi Rufiji wamepatiwa kofia ngumu (helmet) kwa ajili ya kutumia wakiwa kwenye shughuli zao za usafirishaji.

Ugawaji kofia ngumu hizo ulifanyika Desemba 31 mwaka jana, ukiongozwa na Mkuu wa Polisi Jamii Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Ibrahimu katika hafla iliyoratibiwa na Mkaguzi Kata wa Kata ya Mbwara, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Faustina Ndunguru na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Miongoni mwa waliohudhuria ni Diwani wa Kata hiyo, Juma Ligomba pamoja na wananchi na viongozi wengine wa Jeshi la Polisi, huku mgeni rasmi akiwa ni Kaimu Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Rufiji, ACP Grafton Mushi.

Kwa kutambua nafasi ya bodaboda katika kusafirisha abiria, Jeshi la Polisi lilitumia nafasi hiyo kutoa elimu ya usalama barabarani sambamba na elimu ya ushirikishwaji jamii katika kuzuia makosa ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji watoto.

Kata ya Mbwara yenye vijiji vitano, ina wakazi wenye mwamko mkubwa kuhusu uimarishwaji usalama, ikiwamo kufichua uhalifu na wahalifu kutokana na elimu ya mara kwa mara wanayopata kutoka kwa Mkaguzi Kata wa Kata hiyo ya Mbwara ambaye ni Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Faustina Ndunguru.

Mkaguzi huyo Msaidizi wa Polisi amekuwa anaendelea kujenga uhusiano na ushirikiano na wakazi wa vijiji hivyo kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujitambua na kutambua nafasi yao katika kuimarisha ulinzi kwenye jamii yao.

Akizungumzia utoaji helmet hizo kwa bodaboda pamoja na elimu ya usalama barabarani, mkaguzi huyo alisema kuwa kwa muda mrefu bodaboda wamekuwa wakifundishwa masuala kadhaa ya usalama barabarani hususan kuepuka kuendesha kwa mwendokasi pamoja na uchukuaji tahadhari.

Alisema: "Leo hii viongozi wa Jeshi la Polis hapa Rufiji wamefika katika kata hii kukabidhi helmet hizi kwa bodaboda ikiwa ni mwendelezo wa elimu ya usalama barabarani na hasa kama inavyofahamika kuwa helmet ni kitu muhimu kwa bodaboda na abiria wao.

"Hivi karibuni ilitokea ajali ya bodaboda katika kijiji cha Nyamwage ambako bodaboda na abiria wake hawakuvaa helmet na wote walifariki dunia, tukio nililonilazimu kutafuta wadau wa kutoa helmet kwa ajili ya bodaboda ndipo nikaipata kampuni ya... (anataja jina la kampuni|) ikatupa helmet hizi.

Akizungumzia msaada huo kwa niaba ya bodaboda wengine, Katibu wa Bodaboda wa Kata hiyo, Fadhili Liato alipongeza Jeshi la Polisi, akiwamo mkaguzi wa kata hiyo kwa namna anavyoendelea kuwajengea uwezo katika kutambua umuhimu wa kushirikiana katika kudhibiti uhalifu sambamba na makosa ya usalama barabarani.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi funguo, Said Hamad Ramadhani, ni mmoja wa wananchi walionunua nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar, wakati wa hafla ya uzinduzi wa nyumba hizo jana. Kushoto ni Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi: Tutabomoa nyumba zilizochakaa, kuzijenga upya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema nyumba nyingi zilizojengwa na mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar baada ya mapinduzi ya mwaka 1964, zimechakaa na hivyo serikali yake itahakikisha inazibomoa na kuzijenga upya.

Ametaja baadhi ya nyumba hizo zilizojengwa na mwasisi wa mapinduzi ambaye pia ni Rais kwa Kwanza wa Zanzibar, Shekhe Abeid Amani Karume, ni nyumba za Kikwajuni na Kilimani.

Dk. Mwinyi alisema jana kuwa serikali itaendelea kujenga nyumba za kisasa ili wananchi wapate makazi bora na kuyaendeleza maono ya mwasisi huyo katika kuwapatia wananchi maendeleo.

Ni wakati akifungua nyumba za makazi na biashara huko Mombasa, mkoa wa Mjini Magharibu Unguja, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Alisema licha ya nyumba hizo zilizojengwa baada ya mapinduzi kuwa chakavu, miundombinu yake poa imeshaharibika, ikiwamo mifumo ya maji, hivyo serikali itahakikisha inajenga maeneo hayo.

> **Hivyo, aliwasisitiza wananchi kutunza miundombinu hiyo na miundombinu mingine na kuweka mazingira safi ili nyumba hizo kuwa na haiba nzuri na zidumu kwa muda mrefu.**

Alisema serikali pia itajenga nyumba 3,000 katika eneo la Chumbuni, Unguja; nyumba 500 Kikwajuni na majengo hayo yakishakamilika, wananchi watapata mazingira mazuri ya makazi.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuna uhitaji mkubwa wa nyumba za makazi na serikali itaendelea kulipa fidia kwa wananchi wote wa Zanzibar ambao wanapisha miradi ya maendeleo na kushauri watu hao wajengewe nyumba za kisasa kama fidia kwa ajili ya nyumba zao.

Hivyo, aliwasisitiza wananchi kutunza miundombinu hiyo na miundombinu mingine na kuweka mazingira safi ili nyumba hizo kuwa na haiba nzuri na zidumu kwa muda mrefu.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Rahma Kassim Ali, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa miongozo na maelekezo yake na kufanikisha mradi huo.

Alisema bado wanahitaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kutokana na uhitaji mkubwa wa nyumba ili kuendelea kuleta maendeleo hasa katika sekta ya makazi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khadija Khamis Rajab alisema ujenzi wa nyumba hizo za makazi 72 umetekelezwa na kampuni Simba Developar chini ya Mshauri Elekezi Wakala wa Majengo Zanzibar. Ujenzi wake ulianza rasmi Mei 15, 2023 na kukamilika rasmi Oktoba 31, 2024, siku ya mwisho ya mwaka jana.

Alisema eneo hilo lina jumla ya block nne na kila block ina nyumba za makazi 18 na maduka ya biashara ambapo hadi kukamilika kwake, zaidi ya Sh. bilioni tisa zimetumika. Hizo ni fedha za mkopo kutoka Serikali Kuu na tayari nyumba zote zimeshapata wanunuzi.

Alisema tayari watu 29 wameshakamilisha malipo na watakabidhiwa funguo zao na 43 wanaendelea na malipo.

# Bilioni 260/- za CSR Bwawa la Nyerere zinaposuasua miaka minne bila uamuzi

**Na Mwandishi Wetu**




ULIPOANZISHWA tu, ulikutana na hoja kinzani kuhusu hatima ya usalama wa mazingira, lakini uongozi wa juu serikalini ukatolea ufafanuzi kuhusu usalama na faida zinazotarajiwa.

Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP) uko mbioni kukamilika, ukigharimu Sh. trilioni 6.5 hadi kukamilika kwake.

Hata hivyo, kuna mambo yasiyofaa yaliyohusiana na mradi huo yameripotiwa. Mojawapo ni ucheleweshaji utekelezaji miradi ya kijamii kwa zaidi ya miaka minne yenye thamani ya Sh. bilioni 262.34.

Wakati mahitaji ya kitaifa ni mengi, hata kuilazimu serikali kukopa, fedha za miradi ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) zimebaki kwa mkandarasi kwa miaka minne.

Ni hoja iliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kupitia ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23.

Katika ripoti hiyo, CAG anabainisha kuwa kifungu cha 2.1.6 cha Makubaliano ya Utekelezaji Miradi ya Kijamii katika utekelezaji mradi huo, kinaelekeza kuwa, makubaliano ya kina yatajadiliwa na kutiwa saini ndani ya mwezi mmoja baada ya kutiwa saini mkataba wa mradi wa Bwawa la Julius Nyerere.

Kwa mujibu wa mkataba huo, kama ilivyoripotiwa na CAG, mkandarasi ataanza utekelezaji miradi ya kijamii ndani ya mwezi mmoja baada ya kutia saini makubaliano ya kina huku ikizingatiwa malipo ya awali yamelipwa chini ya mkataba wa mradi wa Bwawa la Julius Nyerere.

Kwa mujibu wa mkataba wa utekelezaji mradi wa Bwawa la Julius Nyerere, miradi ya kijamii itatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 262.34 (ikiwa ni asilimia nne ya bei ya mkataba).

Mkataba wa mradi wa Bwawa la Julius Nyerere ulitiwa saini tarehe 12 Desemba 2018 na makubaliano ya kina ya miradi ya kijamii yalipaswa kutiwa saini tarehe 13 Januari 2019.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, Mkataba wa Kina wa Utekelezaji Miradi ya Kijamii ulikuwa haujatiwa saini, ikiwa ni ucheleweshwaji kwa zaidi ya miaka minne (siku 1,610).

Kwa mujibu wa CAG, hali hii ilichangiwa na kuchelewa kuanzisha mazungumzo ya kutia saini Mkataba wa Kina juu ya miradi ya kijamii.

Mdhibiti ana angalizo kwamba, kuchelewa kufikia malengo yaliyokusudiwa kunaashiria hatari ya kushindwa kutekeleza miradi ya kijamii kwa wakati, ikizingatiwa kuwa mradi uko katika hatua ya mwisho za ukamilishaji.

Vilevile, imebainika kuwa, tarehe 16 Desemba 2019, kilifanyika kikao cha majadiliano kuhusu utekelezaji miradi ya kijamii ambapo pande zote zilikubaliana kutekeleza miradi hiyo, hususani ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Dodoma na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Fuga hadi Bwawa la Julius Nyerere.

Hata hivyo, makubaliano haya hayakutiwa saini kutokana na mkandarasi kueleza kuwa miradi iliyopendekezwa haiendani na vigezo vilivyoainishwa katika mkataba wa utekelezaji miradi ya kijamii, kwa kuzingatia aina na utaratibu wa utekelezaji.

Kwa mtazamo wangu, kuna haja kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya watendaji wote waliochangia kutokelezwa matakwa ya kimkataba na kisheria, hata kusabisha zaidi ya Sh. bilioni 260 kutonufaisha wananchi; zikabaki kwa mkanadarasi kwa miaka minne.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambao ndiyo wamiliki wa mradi huo, walipaswa kuwasiliana na Wizara ya Nishati kuhitimisha mvutano kwa kuchagua miradi itakayotekelezwa na mkandarasi.

Pasi na hatua madhubuti kuchukuliwa, kuna hatari mkandarasi akakabidhi mradi wa Bwawa la Julius Nyerere na kuondoka huku wananchi wakishindwa kunufaika na Sh. bilioni 262.34 za uwajibikaji wake kwa jamii (CSR).



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko

## HABARI KITAIFA

# Trafiki wasimamisha na kukagua gari la waziri

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa amesimamishwa na askari wa usalama barabarani na kukaguliwa gari alilokuwa akisafiria lenye namba binafsi katika eneo la Magugu, wilayani Babati, mkoa wa Manyara katika barabara kuu ya Babati-Arusha.

Bashungwa alisimamishwa na askari hao jana eneo la Magugu alipokuwa safarini.

Aliwapongeza askari hao kwa kazi nzuri wanayoifanya huku akisema wawaambie watu barabarani si sehemu ya machinjio ya watu.

Alisema askari hao wanasimamia majukumu yao kwa weledi, hivyo hana budi kuwapongeza.

“Mtu yeyote anayetumia chombo cha moto ni lazima afuate taratibu na sheria za usalama barabarani,” alisema Bashungwa.

Waziri huyo alisema alikuwa amekaa nyuma anaangalia wanavyotimiza majukumu yao, walipomaliza akaona awasalimie kabla ya kuendelea na safari.

Desemba 31 mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan akilihutubia taifa, alisema ajali za barabarani mwaka jana ziliua zaidi ya watu 1,000 na kusisitiza madereva kufuata sheria za usalama barabarani.

Ikumbukwe kuwa kikosi cha usalama barabarani kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka kimekuwa kinafanya ukaguzi wa magari na kimewafungia leseni baadhi ya madereva ambao walikiuka taratibu na sheria za barabarani.



Chemba ya maji machafu ikitiririsha maji machafu katika barabara iliyoko karibu na majengo ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kinamama waliong’ara uchaguzi wa mitaa wataja yaliyowabeba

**Na Grace Mwakalinga**

WANAWAKE waliojitokeza kugombea nafasi mbalimbali kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27 mwaka jana, wameeleza uzoefu wao kwenye harakati za kisiasa, wakitaja uthubutu kama silaha ya kwanza.

Akizungumza katika kongamano lililofanyika jijini Dar es Salaam kujadili ushiriki wa wanawake katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wa Kijiji cha Myegedi kilichopo mkoani Mtwara, Rukia Myachi, alisema alikutana na vikwazo vingi ikiwamo mitazamo potofu kuhusu wanawake kuongoza.

Alieleza kuwa nyingine ni ukatili wa kijinsia, rushwa ya ngono na ukata wa fedha, lakini alijitahidi na kuvumilia hadi kufikia mafanikio.

“Nilikutana na vikwazo vingi, ikiwa ni pamoja na mitazamo potofu kuhusu ushiriki wa wanawake katika kugombea nafasi za uongozi, ukata wa fedha, na ukatili wa kijinsia kama vile rushwa ya ngono, lakini nilivumilia,” alisema Rukia.

**“Nilikutana na vikwazo vingi, ikiwa ni pamoja na mitazamo potofu kuhusu ushiriki wa wanawake katika kugombea nafasi za uongozi, ukata wa fedha, na ukatili wa kijinsia kama vile rushwa ya ngono, lakini nilivumilia,” alisema Rukia.**

Alisisitiza kuwa uvumilivu wake ulithibitisha kwamba wanawake wana uwezo wa kuongoza kwa ufanisi, akawahamasisha wanawake wengine wasiache kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, badala yake wainuke na kuchukua nafasi za maamuzi ili kuwakilisha sauti za wenzao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Tabirugu kilichopo wilayani Kasulu, Mkoa wa Kigoma, Leokadeki Koku, alisisitiza umuhimu wa muungano wa wanawake katika kuleta mabadiliko, akisema wanahitaji kusaidiana na kuhimiza usawa wa kijinsia katika uongozi.

Koku aliongeza kuwa ili wanawake wengi zaidi washike nafasi za uongozi, ni muhimu kuwepo na programu zinazotoa mafunzo ya uongozi kwa vijana, ili kuwawezesha kushiriki katika siasa na kufanikiwa licha ya vikwazo vya kijinsia.

“Najivunia kuwa sehemu ya mabadiliko haya na nimedhamiria kuhamasisha wenzangu kugombea, ili kuleta idadi kubwa ya wanawake katika nafasi za uongozi,” alisema Koku.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mpango wa Mitandao ya Jinsia Tanzania (TGNP), Gemma Akilimali, alieleza furaha yake kuhusu ongezeko la wanawake katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024.

Akilimali alisema kwamba, licha ya changamoto zilizokuwepo, wanawake wengi walifanikiwa kushika nafasi za uongozi katika maeneo yao.

“Nashukuru kuona mwitikio mkubwa wa wanawake kugombea nafasi za uongozi, na kwa mara ya kwanza, wanawake wamepata nafasi ya kuwa viongozi wa vijiji,” alisema Gemma.

Akilimali aliongeza kuwa wanawake 14 kutoka maeneo mbalimbali walifanikiwa kushika nafasi za uenyekiti wa vijiji katika uchaguzi huu.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisisitiza kuwa idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi, hasa ngazi za Serikali za Mitaa, bado ni ndogo.

“Idadi hiyo ni ndogo sana. Lazima tufanye juhudi kubwa zaidi, hasa katika ngazi za Serikali za Mitaa,” alisema Lilian.

Aliwahimiza wanawake kuungana, kubomoa vikwazo vya kijinsia na kushinikiza sera zinazowawezesha kushika nafasi za maamuzi.

Lilian alikumbusha mafanikio yaliyopatikana tangu Mkutano wa Beijing wa mwaka 1995 na kutaja viongozi wa wanawake kama Rais Samia Suluhu Hassan, Spika wa Bunge Anne Makinda, na Dk. Tulia Ackson kama mifano ya mafanikio ya wanawake katika uongozi.

# Vijana wachangia damu hospitali ya wilaya

**Na Steven William,** MUHEZA

VIJANA 20 kutoka kikundi cha Mishemishe, kijijini Mangubu, kata ya Tongwe, wilayani Muheza, mkoani Tanga wamechangia chupa 11 za damu kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Muheza.

Uchangiaji huo uliofanyika hospitalini hapo umeongozwa na Diwani wa Tongwe ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Fani Mussa.

Akizungumza jana, Dk. Mussa aliwapongeza vijana hao kwa kuchangia chupa 11 za damu na kuwataka wawe mabalozi kwa wananchi wengine.

“Uchangiaji wa damu salama ni hiari na ni muhimu kwa sababu katika hospitali yetu tunauhitaji wa damu ili kuokoa wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji, ikiwa huduma za mama na mtoto zinaendelea, uhitaji wa damu salama ni mkubwa,” alisema Mussa.

Alisema wilaya ya Muheza imewekewa malengo na serikali kuchangia damu chupa 1,430 na hadi sasa wamevuka lengo kwa kukusanya chupa 1,694 sawa na asilimia 118.5.

Meneja wa huduma za maabara hospitali hiyo, Doreen Owen, alitoa elimu ya uchangiaji wa damu kwa vijana hao kupima uzito, shinikizo la damu na wingi wa damu.

Mganga Mfawidhi wa Hospital ya Wilaya ya Muheza, Mohamed Zuberi Mzee, alitoa rai kwa wananchi wote kujitokeza kuchangia damu salama ambayo itasaidia kuokoa uhai wa wagonjwa.

Awali, Mhina alisema kujitolea kuchangia damu ni jambo la baraka kwa kuwa linawasaidia wagonjwa wa ajali, wajawazito na watoto.

Alisema hospitali hiyo iko pembezoni mwa barabara kubwa, hivyo inapokea majeruhi pindi ajali inapotokea na kwamba hilo ndilo lililowasukuma kuchangia damu.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Mishemishe, Peter Mwandege, alisema wanachama wake ni wajasiriamali na kwamba wamechangia damu ili wawe sehemu ya kuokoa vifo kwa wagonjwa wanaohitaji damu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ifanyie kazi mapendekezo ya wataalamu kukabili selimundu

**MWANZONI** mwa juma hili, Nipashe ilichapisha ripoti maalumu kuhusu mateso wanayopitia wagonjwa wa selimundu na wazazi wao.

Selimundu (sickle cell anemia), ni moja ya magonjwa ya kurithi yanayoathiri mamilioni ya watu duniani, huku Tanzania, ikiwa ni mojawapo ya nchi zilizoathirika zaidi.

Kila mwaka, zaidi ya watoto 14,000 huzaliwa wakiwa na selimundu nchini, huku idadi kubwa ya wagonjwa hao wakitokea katika maeneo ya Kanda ya Ziwa.

Ugonjwa huu, ingawa unajulikana na kupokewa kama changamoto ya kiafya, bado unaleta madhara makubwa kwa watoto na familia zao kwa sababu ya uelewa mdogo, gharama kubwa za matibabu na changamoto za kijamii na kiuchumi zinazozunguka ugonjwa huu.

Selimundu ni ugonjwa wa damu unaosababishwa na mabadiliko katika vinasaba vya mtu, ambapo seli nyekundu za damu hubadilika na kuwa na umbo la mundu badala ya umbo la duara.

Hali hii husababisha ugumu wa damu kupita kwenye mishipa ya damu, hivyo kusababisha maumivu makali, majeraha ya viungo, upungufu wa damu na hatari ya magonjwa mengine kama kiharusi.

Watoto wanaozaliwa na selimundu wanahitaji matibabu ya mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na kuongeza damu, kutumia dawa za kuzuia magonjwa nyemelezi na dawa aina ya Hydroxyurea ambayo husaidia kupunguza uwezekano wa kupata kiharusi na kuzuia damu kuwa nyepesi.

Hata hivyo, matibabu haya ni ya gharama kubwa, na wengi wanashindwa kumudu.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 75 ya watoto wanaozaliwa na selimundu duniani wanatoka Afrika, na Tanzania ni nchi ya tatu barani kwa idadi kubwa ya wagonjwa.

Wengi wa wagonjwa na familia zao hujua tu kuhusu hali ya ugonjwa baada ya mtoto kuzaliwa na kugundulika kuwa na tatizo hili.

Hali hii inafanya matibabu kuwa vigumu, kwani wengi wanakuwa hawana uelewa wa kutosha wa jinsi ya kukabiliana na ugonjwa huo. Nipashe Jumapili tunaungana na mabingwa wa selimundu nchini kushauri watu wapime vinasaba vyao kabla ya kuoana, ili kuepuka kuzaa watoto wenye ugonjwa huu.

Hii ni njia moja ya kupunguza mzigo wa kifedha na kijamii unaotokana na matibabu ya watoto wenye selimundu.

Tiba ya selimundu ni kupandikiza uloto, lakini ni mchakato wa gharama kubwa na unaohitaji msaada wa kifedha kutoka kwa serikali. Ili kukabili selimundu serikali italazimika kutenga Sh. bilioni 770 kila mwaka kwa ajili ya matibabu ya watoto 14,000 wanaozaliwa na selimundu.

Matatizo haya hayaji tu kwa upande wa kifedha, bali pia kwa upande wa kijamii. Familia nyingi zinaishi katika hali ngumu baada ya mtoto wao kugundulika kuwa na selimundu.


Mifano ya wazazi waliopoteza watoto wao kwa sababu ya ugonjwa huu, kama walivyonukuliwa na Nipashe mwanzoni mwa wiki, inaonesha wazi namna ugonjwa unavyohusiana na hali ya kifedha na kijamii.

Hivyo, elimu kuhusu selimundu inapaswa kupewa kipaumbele, na serikali ina jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huu. Ili kukabiliana na ugonjwa huu, ni muhimu pia kuwa na sera za kitaifa na sheria zitakazowataka watu kupima vinasaba vyao kabla ya kuoana kama ilivyopendezwa na mabingwa wa selimundu waliozungumza na Nipashe.

Hii itasaidia kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa na ugonjwa huu, na hivyo kupunguza mateso ya kijamii na kiuchumi yanayozunguka ugonjwa huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mitungi ya gesi iuzwe kwa bei rafiki kuokoa mazingira

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya mikakati ya serikali katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwa mwaka 2024/25 ni kugawa mitungi ya gesi yenye thamani ya Sh. bilioni 10.

Naibu Waziri Nishati, Judith Kapinga anasema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika mwaka huu wa fedha imepanga kutoa mitungu 400,000 kwa wananchi yenye thamani ya kiasi hicho cha fedha.

Kwa mujibu wa Judith, lengo la serikali ni kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utunzaji mazingira na kuwaepusha wananchi na maradhi ambayo yanatokana na matumizi ya nishati isiyo safi.

Nipongeze serikali kwa mkakati huu wa kutunza mazingira na kuwaepusha wananchi wake dhidi ya maradhi yatokanayo na mtumizi ya kuni na mkaa.

Nia ya serikali ya kupunguza gharama za vifaa vya nishati safi ya kupikia ni nzuri, lakini ninadhani kungekuwa na bei elekezi ambayo haimuumizi mtumiaji wa hali ya chini.

Kwa sasa kujaza gesi katika mitungi midogo ni kati ya Sh. 23,000 hadi 24,000 ambazo ninaamini watu wa hali ya chini huenda wasimudu bei.

Kwa mfano, vijijini unaweza kukuta mji una zaidi ya watu 10, kwa idadi hii ya wanafamilia, ni wazi matumizi ya gesi yatakuwa makubwa lakini kutokana na hali ya maisha huenda wakakwama kutumia gesi na kurejea kwenye kuni au mkaa.

Hivyo, suala la unafuu wa bei ya gesi lipewe uzito huku wauzaji nao wakidhibitiwa ili wasipandishe bei na kuwaumiza watumiaji wa hali ya chini.

> **Hivyo, suala la unafuu wa bei ya gesi lipewe uzito huku wauzaji nao wakidhibitiwa ili wasipandishe bei na kuwaumiza watumiaji wa hali ya chini.**

Ninaamini kuwa familia inapokuwa kubwa, mtumizi ya gesi nayo yanakuwa makubwa. Kama nilivyoeleza, watu wa vijijini ambao kwa miaka yote wanatumia kuni, kuna uwezekano wakashindwa kumudu gharama za mitungi ya gesi.

Uzoefu unaonesha kuwa imekuwa ni kawaida kwa wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali kupandisha bei ya bidhaa kiholela na kusababisha kuwapo ugumu wa maisha kwa watu wa hali ya chini.

Hata kwenye mitungi ya gesi wanaweza kufanya hivyo na kusababisha kile ambacho serikali imekikusudia kwa wananchi wake kisifikie malengo.

Hivyo, mikakati wa kudhibiiti uharibifu wa mazingira utafanikiwa ikiwa serikali itahakikisha bei ya gesi inakuwa rafiki kwa kila mtumiaji mijini au vijijini.

Hivi sasa hali si nzuri kwa upande wa mazingira.

Wakata mkaa ni shida kubwa katika mikoa mbalimbali kwa kuwa kila kukicha maelfu ya magunia ya mkaa yamekuwa yakipelekwa jijini Dar es Salaam.

Bila kuchukua hatua kama hizo ambazo serikali inafanya za kuelekeza nguvu katika matumizi ya nishati safi, tunajiandaa kuwa na jangwa.

Kwa kuwa Tanzania ina gesi, ni vyema bei yake ikawa ni ya kawaida, wafanyabiashara wasiuze kwa bei ya 'kukomoa' ambayo itasababisha watu kutamani kurudi kwenye kuni na mkaa ambavyo vinaharibu mazingira.

Tusikubali kuendelea kushuhudia nchi nzima mapori yakifyekwa kwa ajili ya mkaa na kuni, badala yake gesi itumike kuokoa misitu, lakini iwe na bei ambayo kila mtu ana uwezo wa kuimudu.

MAKALA

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mwanamuziki akihama Sikinde, wimbo aliouacha unarekodiwa



Na Adam Fungamwango

ORCHESTRA Mlimani Park, wakati huo ikimilikiwa na Umoja wa Madereva Taxi nchini Tanzania, baadaye ikaitwa DDC Mlimani Park, ilipochukuliwa na Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam. Kwa sasa inaitwa Mlimani Park Orchestra, na hii ni baada ya wanamuziki kujitoa kwenye shirika hilo na kujitegemea yenyewe.

Mtindo wake tangu ianzishwe mwaka 1978, ni 'Sikinde Ngoma ya Ukae'. Pamoja na kwamba ilianzishwa mwaka 1978, kutokana na asilimia 80 ya wanamuziki kutoka Dar International, lakini iliondokea kuwa tishio kwa bendi zote ambazo ilizikuta.

Ikawa ndiyo mpinzani wa jadi wa bendi kongwe ya Juwata Jazz Band, badala ya Urafiki Jazz. Sikinde ilishawahi kutwaa ubingwa wa muziki Tanzania katikati ya miaka ya 1980, kwenye mashindano ya muziki wa dansi Tanzania (MASHIBOTA).

Hadi leo, bendi hiyo na Msondo Ngoma Music, ndizo zinazohesabiwa kuwa ni bendi kubwa zaidi na nembo ya muziki wa Tanzania.

Msondo yenyewe ilianzishwa mwaka 1964, ikiitwa NUTA Jazz, baadaye Juwata Jazz, ikaja kuwa OTTU Jazz, ikitumia mtindo wa Msondo Ngoma, ambao baadaye ikawa ndiyo jina la bendi, baada ya wanamuziki kuanza kujitegemea wenyewe kutoka kumilikiwa na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini.

Sikinde ni bendi iliyorekodi nyimbo nyingi ndani na nje ya nchi, ambazo zilipendwa na zinaendelea kupendwa na vizazi vyote vitakavyokuja.

Hata hivyo kuna jambo ambalo baadhi ya mashabiki wa muziki hawalijui. Sikinde ni bendi ambayo ilirekodi nyimbo kadhaa ambazo zilitungwa na wanamuziki wake waliohama.

Wao hawakuona tabu kurekodi wimbo wa mwanamuziki wake ambaye amehama.

Mara nyingi zamani mwanamuziki anaweza akawa ametunga na kuufanyia mazoezi wimbo fulani, halafu kwa bahati mbaya au nzuri ameihama bendi hiyo, basi wengi huondoka nao. Na bendi ambayo ameondoka huwa haijishughulishi tena na wimbo huo. Badala yake mwanamuziki huyo anaupeleka kule alikohamia na kurekodi.

Hii imetokea mara nyingi na wiki ijayo nitaziorodhesha baadhi ya nyimbo za bendi kadhaa ambazo kabla zilikuwa kwenye bendi zingine.

Utashangaa kuwa wimbo wa bendi hii ambao unaufahamu ulitungwa na kuimbwa mpaka jukwaani na bendi nyingine, lakini mtunzi alihama, akaondoka na wimbo wake, kuupeleka bendi nyingine.

Lakini Sikinde haikuwa hivyo. Wao ukiondoka, wanakwenda kurekodi. Na hii iliwasababisha mzozo na baadhi ya bendi na wanamuziki wake.

Ndiyo maana kuna nyimbo kadhaa za Sikinde, ambazo pia zimerekodiwa na bendi zingine.

Tukianza na wimbo wa 'Nalala kwa Tabu'. Huu ulitungwa na Cosmas Thobias Chidumule, mwanzoni mwa miaka ya 1980. Kabla ya kuurekodi kwenye studio za Redio Tanzania Dar es Salaam, alihama na kujiunga na Vijana Jazz Band.

Sikinde kwa kujua kuwa mtunzi wa wimbo huo amehama, hawakumuachia aende nao, walipokwenda kurekodi waurekodi, ingawa kwa uungwana wakaandika mtunzi ni Chidumule, ingawa hayupo.

Hapa sasa haikujuliana kama Vijana Jazz chini ya uongozi wa Hemed Maneti, hawakuoana umuhimu na wao kuurekodi wimbo huo, au Chidumule hakuupeleka.

Huenda ikawa hakuupeleka ili kuonyesha ana hazina ya nyimbo, kwani ni kipindi hicho hicho akiwa bendi yake mpya wa Vijana Jazz, alichotunga na kurekodi nyimbo, ambazo ni 'Nilitaka Iwe Siri', "Maisha Ni Safari Ndefu', na 'Unikubalie'.

Uongozi wa DDC Mlimani Park ulishtushwa na kushangazwa na uwezo mkubwa wa Chidumule, kwani nyimbo hizo tatu alizotunga Vijana Jazz zilitikisa nchi na kuibeba mno bendi hiyo, huku wimbo aliouacha Sikinde nao ukionekana kupendwa mno na mashabiki. Ilibidi wapande nao na kumrudisha, licha ya kwamba aliondoka kwa 'figisu'.

Chidumule huyo huyo, katikati ya miaka ya 1980, alikwenda bendi ya Kurugenzi Jazz Band na kutunga wimbo wa 'Majirani Huzima Redio', lakini muda mfupi baadaye alirejea Sikinde na pia akaurekodi wimbo huo. Kwa maana hiyo wimbo wa 'Majirani Huzima Redio' upo wa Kurugenzi Jazz Band na wa Sikinde, ingawa huu ni mwenyewe Chidumule aliamua kurekodi huku na huku.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Sikinde ilimpokea mwanamuziki Ramadhani Kinguti 'System'.

Akawatunga wimbo unaitwa 'Majirani Huzima Redio'. Kabla ya kurekodiwa, akahama. Kwa kawaida ilibidi ahame nao. Sikinde wao walikwenda kurekodi RTD, wakarekodi na wimbo huo, mtunzi akiwa ameshaondoka. Ilileta mzozo.

Mtunzi wa wimbo huo, Kinguti naye akaurekodi akiwa kwenye bendi aliyohamia ya Bicco Stars. Hadi leo nyimbo hizo zipo mbili. Wa Sikinde na wa Bicco.

Mwanzoni mwa mwaka 2000, mwanamuziki Hussein Jumbe akiwa na bendi hiyo alitunga wimbo wa 'Nani Kauona Mwaka'. Kabla hajarekodi na Sikinde, akanyakuliwa na TOT Plus Band. Akaondoka nao. Huku nyuma, Sikinde wakaenda kuurekodi RTD. Jumbe hakukubali kwa sababu ni wimbo wake. Naye akaenda kuurekodi akiwa na TOP Plus. Huku akauita, 'Nani Kaiona Kesho'. Kwa hiyo nyimbo hizo zipo mbili, wa Sikinde na wa TOT Plus Band.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Mkutano wa kimataifa wa nishati waiva

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Afrika Kuhusu Nishati ulioandaliwa mahsusi kwa ajili ya uhamasishaji matumizi ya nishati safi duniani, ukipangwa kufanyika Januari 27-28 mwaka huu.

Mkutano huo unaotarajiwa kufanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, ukichagizwa na utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa kinara katika uhamasishaji matumizi ya nishati safi ya kupikia Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

Akizungumzia mkutano huo juzi, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alisema ni heshima kubwa kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ambao mataifa ya Afrika yamevutiwa kwa namna Tanzania ilivyofanikiwa kwenye usambazaji umeme vijijini na vitongojini.

Msigwa alisema wageni hao wanakuja kuangalia Tanzania imefanikiwaje kusambaza umeme katika vijiji vyote nchini.

"Wanakuja kwa sababu Tanzania inafanya vizuri kwenye nishati, na hasa kwenye usambazaj umeme, na kampeni kubwa ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anaifanya kuhamasisha watanzania kutumia nishati safi ya kupikia," alisema Msigwa.

Desemba 31 mwaka jana, akiwa wilayani wilayani Ruangwa, mkoani Lindi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwataka watanzania kumuunga mkono Rais Samia kwa kutumia nishati safi.

"Matumizi ya nishati safi ambayo ni gesi, umeme pamoja na makaa ya mawe, yanalinda afya ya watanzania, yanalinda mazingira dhidi ya ukataji miti pamoja na kutoa ulinzi kwenye nishati endelevu," alisema Majaliwa.

Akiwa New York, Marekani Septemba, mwaka jana, kwenye mkutano wa kujadili ajenda ya upatikanaji nishati Afrika, Waziri Mkuu alisema pamoja na mambo mengine, mkutano huo utajadili namna ya kukusanya dola za Marekani bilioni 190 ili zitumike kufikisha umeme kwa wananchi milioni 300 barani humo ifikapo mwaka 2030.



Mwendesha baiskeli akiwa amefunga mzigo mkubwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HABARI PICHANI



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na Mkewe, Mama Mariam Mwinyi, wakimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar, Sultan Said Suleiman, akitoa maelezo ya kitaalam kuhusu ujenzi wa nyumba 72 za shirika hilo zilizojengwa katika eneo la Mombasa Kwamchina, wilaya ya Magharibi "B" Unguja, ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar jana. **PICHA ZOTE: IKULU**




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussein Ali Mwinyi, akifungua pazia kuweka jiwe la msingi la ufunguzi wa nyumba 72 za makazi na biashara za Shirika la Nyumba Zanzibar jana.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akielekea katika sehemu iliyoandaliwa kwa ajili ya kuzungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi la ufunguzi wa nyumba hizo.



Vijana wa hamasa wakishangilia wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na wananchi wakati wa hafla ya uzinduzi wa nyumba hizo.



Baadhi ya mawaziri na wageni waalikwa wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa uzinduzi wa nyumba hizo za makaazi na biashara.



Baadhi ya wananchi wa mkoa wa Mjini Magharibi Unguja wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi wakati wa uzinduzi wa nyumba hizo.


# MAISHA

JANUARI 5, 2025

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*

## HARUSI

Ukurasa 12





# Tengeneza tumbo la nyigu

Ukurasa 14

## WATOTO

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| I | T | A | L | Y | |
| | O | | I | | I |
| | G | A | B | O | N |
| | O | | Y | | D |
| | | M | A | L | I |
| | | | | | A |


### FUMBO TOTO

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

DOA, WAO, LAO, TIN, JUNGU, IKOME, NONDO, TOLEO, UBWABWA, BWAWANI



### TOA TOFAUTI 5





### AMSHA AKILI

JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | 4 | | 1 |
| | | | 2 |
| 3 | | | |
| | | | 3 |

## PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanangu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mwanamume usikubali katu kulishwa na mwanamke!

HERI ya Mwaka Mpya msomaji wangu. Tumshukuru sana Mungu kwa uhai huu aliotukarimu kwa upendo wake mwingi. Tunaendelea kumulika anga la wanaume.

Makala ya mwisho mwaka jana, tulianza kuangalia mambo ya msingi wanayopaswa kuzingatia wanaume katika nafasi zao kama baba wa familia.

Nikasema kuna kitu kikubwa sana Mungu anatarajia kwa kina baba. Mungu ana wathamini, hivyo msimwangushe. Mungu alimuumba mwanamume kwa kumwamini. Alimpa nafasi ya kwanza kupokea pumzi!

Hiyo ilikuwa nafasi ya kipekee kwa mwanamume. Hata siku moja usijute eti kwa nini Mungu alikuumba mwanamume, alikuthamini. Alikuumba kwa kusudi maalumu.

Baada ya kumuumba alimpa kazi/majukumu kwenye bustani ya Eden. Aliyepewa kazi na maelekezo ni mwanamume. Kwa mantiki hiyo, mwanamume usioe kabla ya kazi utakwama.

Naam, ili sasa mwanamume huyu asimwangushe Mungu nilitaja baadhi ya mambo ya msingi ya kuzingatia; kuwa mstari wa mbele kwa mambo ya Mungu. Hapaswi kuwa mbali na Mungu.

Kingine nikataja ahakikishe anafanya kazi kwa bidii. Kabla ya mwanamke Mungu alimpa mwanamume kazi. Wanawake wamekuwa chanzo cha wanaume kuathiriwa ndani ya ndoa.

Leo twende zaidi kumtahadharisha mwanamume awapo katika ndoa yake. Usikubali kulishwa na mwanamke kwani ataishia kukudharau. Siku ukila chakula cha mwanamke ambacho hujakitolea fedha ya matumizi, kimbia!

Unaweza kujikuta yupo mwanamume nyuma yako, ipo picha ya mwanamume mwingine, ndiye anatoa matumizi nyumbani kwako. Usikubali kula chakula cha bure. Wanawake hawajaumbiwa kutoa bali kupokea!

Mwanamke ukitaka kupata fedha toka kwa baba (mume), tumia mbinu. Na mwanamke akitoka afanye kazi na asirudi nyumbani mikono mitupu. Mwanamke aneyejitambua harudi nyumbani mikono mitupu.

Pointi nyingine ili mwanamume asimwangushe Mungu, hakikisha unalima. Wapo baadhi ya wanaume huwaachia wanawake kazi zote. Kazi nyingine ya mwanamume ni kutunza/kulinda.

Hakikisha mnawalinda wote walio chini yenu. Mengi yanatokea kwenye familia, kisa baba hawatambui jukumu lao. Kwa mfano, mwanamume akiomba heshima kwa mkewe, kuna shida kwani heshima haiombwi!

Mwanamke anapohisi kushambuliwa hutoa sumu zote mwilini. Mwanamke anapohisi halindwi aweza kuwa chochote. Kazi ya kuatamia ni ya baba!

Wanawake kwa asili wana wivu wanapohisi kuna mtu anaingilia anga lao. Na mwanamke akianza kulipa kisasi, hata shetani hukaa pembeni anachukua taarifa.

Linda mke wako, usiruhusu mume aungane na ndugu zake kumshambulia mke. Linda familia yako! Unaweza kumhudumia mke wako unavyotaka wewe kwani huyo ni wako.

Mwanamke huhamisha moyo. Unaweza kufikiri una mke kumbe alishahama. Humsemeshi mwenzio wiki nzima, akipata kidumu nje utakoma. Yaliyowakuta wanalifahamu hilo.

Mungu katika neno lake anaagiza; Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu (Waefeso 5:22). Kwa asili mwanamke anatii pale anapoona kitu.

Wapo ambao hawatii waume zao kama baba zao wa kiroho. Wanawake wanapaswa kupunguza jeuri kwani mume ni kichwa cha mkewe.

Mtu aweza kujiuliza; kwa nini wanawake hawana utii kwa waume zao? Jibu ni kuwa hawana upendo. Ukweli ni kwamba tunahitajiana, kila mmoja akifanya sehemu yake kila kitu kitakwenda sawa.

Neno la Mungu linatoa angalizo kuwa; 1Petro 3:7 "Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu. maombi yenu yasije kuzuiliwa".

Mwite jambo linapotokea, badala ya kutulia, unakasirika. Unapokosea usitumie ubabe, eti mimi ni mwanamume. Nyuma ya kila mwanamume aliyefanikiwa yupo mwanamke aliyesimama. Hali kadhalika katika kuanguka.

Mwanamume usimfanye mwanamke agumie maumivu ndani ya moyo. Ishi na mwanamke kwa akili, maombi yako yasije kuzuiliwa. Kama hukumlinda akawa na sumu ndani, analia huwezi kupenya!

Wanawake wengi wamekandamizwa na waume zao. Usimlinganishe mume wa mwenzio na yule wa kwako kwani uwezo unatofautiana.

Usimseme mkeo kwa watu, mlinde asijue. Makahaba wengi wanamshambulia mke kwa kuwa mwanamume amewapa nguvu. Anamchokoza yule aliyemlipia mahari.

Mwanamke anamwambia mume hao wanawake zako waambie waache kunishambulia. Lakini bado anapuuzia kwa kuwa amewapa nguvu na kuwa karibu nao kuliko mke.

Kingine mfundishe mkeo. Wakati Mungu anampa Adamu maelekezo, mwanamke hakuwapo. Usimseme kwa watu, usimtolee mifano.

Hakuna familia iliyokamilika, elewa kinachomsibu mwenzako, usimsemeseme. Kinachotokea kwenye familia msikiseme.

***Je, una maoni? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Uchaguzi CHADEMA, mantiki si kujiamini ni kuaminika

UJINGA hauondoki kwa kumchukia mwenye akili, wala kuhesabu dhambi za mwenzio hakukufanyi wewe kuwa mtakatifu.

Kuna shida kubwa naiona kwa wanasiasa wetu. Wengi hawajui dhana ya mtu kujiamini lakini asiaminike.

Kuna mtu kujiamini na kuaminika. Kiongozi mzuri anatakiwa kujiamini na kuaminika; ila mtawala anaweza kuwa yeyote mradi anajiamini.

Mwanasiasa ana ndimi nyingi, ana sura nyingi, hata kama ni mwanasiasa makini. Anaweza kutumia umakini wake kuteka fursa za kisiasa.

Kila anachokitafakari, anachokiandika, achokifanya na anachokitamka, analenga kutafuta na kupata fursa binafsi kwa wakati huo au baadaye.

Mtu wa aina hiyo ni msaka fursa. Kwa sababu hiyo ana ndimi nyingi, ana sura nyingi. Lengo ni kutaka anachokitaka.

Watu wenye hekima, huweka katika taasisi zao, iwe kwa kuchagua au kuteua viongozi wanaojiamini na kuaminika.

Huko CHADEMA moto unawaka. Wafuasi wa wagombea wawili wenye nguvu wanaparurana, wanachafuana ili kutwaa madaraka.

Kuna mmoja anayejiamini na kuaminika; na kuna mtu anayejiamini lakini haaminiki.

Je, ni kweli mmoja wao kati ya wanaoimbwa kila uchao mitandaoni na kwenye vyombo vya habari, anaweza kupata shida kufanya kazi na Kamati Kuu ya CHADEMA kama akishinda?

Nimesikiliza mahojiano maalumu ambayo mwanazuoni Prof. Azaveli Lwaitama,alifanya na mwanahabari mmoja kuhusu uchaguzi wa Mwenyekiti wa CHADEMA.

Katika mahojiano yale aligusia mambo mengi na Waraka wa Ndani leo unakijikita kwenye kipengele kimoja kinachohusu Kamati Kuu.

> **Mwanasiasa ana ndimi nyingi, ana sura nyingi, hata kama ni mwanasiasa makini. Anaweza kutumia umakini wake kuteka fursa za kisiasa.**

Katika hoja yake, Prof. Lwaitama amenukuliwa akisema kama mgombea mmoja atachaguliwa kuwa mwenyekiti, anaweza kupata shida kufanya kazi na Kamati Kuu, kwa kuwa wajumbe wa Kamati Kuu, wengi wao ndio waliomsindikiza mmoja wa wagombea wakati akitangaza nia ya kugombea na wakati anachukua fomu.

Prof. Lwaitama, akasema kati ya wajumbe wa Kamati Kuu, ambao ni kama 24; ni wajumbe watano pekee ndiyo watatokana na uchaguzi huo.

Bila kujali anachaguliwa nani katika uchaguzi huo, ieleweke kwamba wanazuoni wetu ambao wamejijengea heshima kubwa miongoni mwa jamii, moja ya majukumu yao ya msingi ni kushahijisha mijadala katika jamii ili kutoa mwelekeo wa uamuzi sahihi. Namuunga mkono!

Hoja yangu ni hii; mtu yeyote atakayechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA, anayo nafasi kubwa ya kuidhibiti Kamati Kuu na kufanya kazi nayo vizuri.

Kwanza, hadi sasa hakuna uthibitisho wa kimantiki kuhusu ni nani kati ya hao vigogo wawili wa chama kikuu cha upinzani nchini, anayo nafasi ya kuithibiti Kamati Kuu ijayo.

Mantiki yangu hapa ni kwamba mwenyekiti atakayechaguliwa ndiye atakayeidhibiti kwa kuwa mchakato wa kuikamilisha utamtegemea yeye.

Wajumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA baada ya uchaguzi huo hawatapungua 30.

Kati ya wajumbe waliopo sasa, wengine wote watakoma kuwa wajumbe siku ya mkutano mkuu wa uchaguzi, hivyo watabaki wajumbe 10 tu ambao ni wenyeviti wa kanda. Wajumbe wengine 20 au 21 watatokana na uchaguzi huo.

Kwa mantiki hiyo, idadi ya wajumbe wa Kamati Kuu watakaotokana na uchaguzi huo ni sawa na theluthi mbili (67%).

Kwa mantiki hiyo, mwenyekiti yeyote ambaye atachaguliwa anayo nafasi kubwa ya kuwa na udhibiti wa Kamati Kuu, kwa vile kati ya hao, wanane anawateua mwenyewe.

Ni wazi kuwa uchaguzi wa kupata Mwenyekiti wa CHADEMA, safari hii umevuta hisia za walio wengi, wakiwamo marafiki na maadui zao.

Ninyi ni mashahidi huko mitandaoni, mijadala ni mingi, wanakosoana kwa jazba, wanadhalilishana, wanabwaga hadharani siri za chama chao na wameingia mtego uleule wa makundi, ambao wapinzani wao wamekuwa wanautumia na kuwaparaganyisha kabla ya uchaguzi.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



Ulikuwa usiku wa kukumbukwa kwa Dk. Ally na mke wake Sabra baada ya kufunga ndoa hivi karibuni. PICHA: MC GaraB

MITINDO

N[illegible]i Lusonzo



# CHEONGSAM ZAIDI YA VAZI

KWA Wanawake ambao wanataka kuwa tofauti mwaka 2025, unatakiwa kuwa miongoni mwa wavaaji wa nguo ya Cheongsam.

Cheongsam ni vazi lenye asili ya China, lakini kutokana na uzuri wake limeanza kusambaa sehemu mbalimbali duniani.

Baadhi ya waliofanikiwa kuvaa wameelezea jinsi nguo hiyo ilivyowapa tofauti mkubwa na kuonekana wenye mvuto wa kipekee.

Nguo hizi zimetengenezwa kwa kitambaa laini cha satini ambacho humfanya mtu kuwa na raha pale anapovaa.

Kimsingi Cheongsam imetengenezwa kwa kitambaa kisafi na kikavu kwa ajili ya kulinda afya ya mvaaji.

Jambo zuri vazi hili lina mitindo ya aina nyingi na hata wale wanaopenda mipasuko hawajatengwa kwani kuna aina mbalimbali za mipasuo.

Vazi hili linafaa kuvaliwa sehemu mbalimbali kama sherehe za harusi, ofisini na hafla mbalimbali za kijamii.

**Picha zote: Pinterest**

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Tengeneza tumbo la nyigu



KILA mwanamke anatamani kuwa na umbo zuri, lenye mikatiko ya kike ambao unamvutia kila mtu.

Moja ya kiungo ambacho kinabeba mwonekano mzuri wa mwanamke nit umbo dogo.

Mwanamke akiwa na tumbo kubwa inapoteza mwonekano wake, badala yake anahitaji kufanya jitihada kubwa kurudi katika umbo lake la awali.

Ukubwa wa tumbo unatokana na mrundikano wa mafuta tumboni kutokana na aina ya maisha ya kisasa.

Kama una tatizo hilo, hizi ni baadhi ya njia ambazo zitakusaidia kuwa na tumbo dogo

**Chai ya rangi**

Chai ya rangi huwa na kemikali muhimu ya kuunguza mafuta ya tumbo ambayo huitwa epigallocatechin gallate.

Kemikali hizi kwa miaka mingi zimekuwa zinatumika katika kutengeneza vyakula na vinywaji kwa ajili ya watu wanaotaka kupunguza tumbo.

Ufanisi wake huongezeka zaidi kwa watu wanaofanya mazoezi, pia ikichanganywa na limao au ndimu.

**'Apple cider vinegar'**

Umewahi kwenda supermarket ukakutana na chupa imeandikwa kwa majina hayo?

Hiyo chupa ni chaguo sahihi kwa watu wenye tumbo kubwa.

Siki ya tufaa inakemikali za acetic acid ambazo tafiti nyingi zinathibitisha uwezo wake wa kuunguza mafuta ya tumbo.

Kiasi cha vijiko viwili kwa siku vilivyo changanywa kwenye maji vinatosha kabisa kuleta majibu chanya.

**Usingizi**

Kulala muda mrefu ni afya, hakikisha unalala kwa saa 9 hadi 12 kwa siku ili kupunguza tumbo.

Usingizi ni dawa njema pia kwa afya ya mwili na akili, ukifanya hivyo utapunguza kitambi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Keki ya Chocolate

JE unataka kutengeneza keki na kula nyumbani na familia yako? Basi usipate shida nataka kukupa njia ya kuoka keki tamu ya Chocolate.

Keki ya aina hii ina radha nzuri na inapendwa kuliwa na kila mtu.

**MAHITAJI**

Unga wa ngano vikombe viwili, sukari vikombe viwili, cocoa robo tatu ya kikombe na baking powder vijiko vya chai viwili .

Mahitaji mengine ni baking soda kijiko kimoja na nusu cha chai, espresso powder kijiko kimoja cha chai, maziwa kikombe kimoja, mafuta nusu kikombe, mayai mawili, chumvi kijiko kimoja na na maji ya moto kikombe kimoja

**NAMNA YA KUPIKA**

Weka jiko au oven lenye nyuzi joto 350, vyombo unavyotumia kuoka keki vipake mafuta kisha weka pembeni.

Weka unga, sukari, cocoa, baking powder, baking soda, chumvi na espresso powder kwenye bakuli moja.

Changanya vizuri mpaka mchanganyiko uchanganyikane vizuri.

Ongeza maziwa, mafuta na mayai kwenye mchanganyiko wa unga.

Changanya mpaka iwe vizuri na kuongeza maji ya moto kisha changanya kwa dakika mbili.

Weka mchanganyiko kwenye chombo cha kuokea, oka kwa dakika 30 mpaka 35.

Epua chukua toothpick choma katikati kujua kama keki imeiva vizuri. Ikiwa tayari iache kwa dakika 10 ipoe.

Itoe kwenye chombo cha kuokea kisha itakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa muda wowote.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Msimu wa kutafuta nyumba umewadia, zingatia haya

MSIMU wa kutafuta nyumba za kuishi umewadia. Ni vema katika kipindi hiki kuwa makini zaidi katika kutafuta nyumba ambayo haitakuletea shida, hakikisha hukurupuki.

Hakikisha unazingatia mambo muhimu kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho wa kupanga nyumba kwa ajili ya kuishi.

Mojawapo ya mambo ya kuangalia ni mahali nyumba ilipo na umbali, kumbuka kuna uwezekano mkubwa ukaona nyumba nzuri kwa mwonekano na ukatamani upange kwa ajili ya kuishi, lakini ikawa iko mbali zaidi au ikakulazimu kutumia fedha zaidi kwa upande wa usafiri.

Kwamba, endapo unatumia usafiri wa umma, ikakulazimu kila ukifika kituoni ni lazima utumie tena usafiri mwingine ambao nao ni gharama kubwa kufika kwenye nyumba hiyo, hivyo ni lazima ufikirie kwa makini kufikia uamuzi wa kuishi kwenye nyumba hiyo la sivyo unaweza ukashindwa kuweka akiba kwa ajili ya kufanyia maendeleo mengine.

Jambo lingine la muhimu la kuangalia kabla ya kupanga nyumba ni kuangalia kama nyumba hiyo itahitaji marekebisho makubwa.

Kuna baadhi ya nyumba zinakuwa zinaonekana vizuri kwa nje, lakini ndani zinakuwa zinahitaji marekebisho makubwa ambayo huenda yakakuongezea gharama kubwa za ambazo hukutegemea.





Kwahiyo inabidi ujiulize kama kuna ulazima wa kuishi kwenye nyumba hiyo au kama unaweza kutafuta nyingine na ukaepuka hayo isipokuwa tu kama mmiliki yuko tayari kurekebisha kwa gharama zake mwenyewe.

Lingine ni masharti yanayokuwa yamewekwa kwenye nyumba husika. Baadhi ya wenye nyumba huweka masharti magumu na wakati mwingine mpangaji anapofika kuhitaji nyumba hawasemi ukweli na badala yake baada ya kulipa na kuanza kuishi ndipo huanza kuyasema kidogo kidogo kwa wapangaji, hivyo ni vema kudodosa hilo kabla ya kufikia uamuzi wowote.

Hakikisha unasoma kwa makini mkataba kabla ya kulipia pesa yako kwenye nyumba. Wengi hufikiri ukishalipa kodi basi hakuna jambo la kwenda vibaya, lakini mambo yanaweza kubadilika.

Kama ambavyo unakubali kwa kuandika kwamba utalipa kodi kwa wakati na kuitunza vyema, hakikisha pia na mkataba wako unausoma vizuri na kama kuna mambo ambayo mwenye nyumba anapaswa kuyatekeleza anafanya hivo, kama ilivyo kwako na kama ukibaini kama kuna kitu kinakufunga ni bora uulize mapema kabla ya kuingia rasmi kwenye nyumba.

Pia huu ni msimu wa mvua, hakikisha unazingatia endapo eneo la nyumba iliyopo hapajai maji, kwa sababu hilo nalo ni tatizo jingine linaloweza kukuletea shida.

# Tengeneza bustani yako kimkakati

Na Restuta James

UNAHITAJI hewa safi ya oksijeni, kupunguza msongo wa mawazo na kuleta utulivu nyumbani kwako mwaka huu?

Kama jibu lako ni ndiyo, basi zingatia maelekezo ya makala haya ya bustani, ujue mbinu za kukupa utulivu wa nafsi na akili katika mwaka huu na mingine ijayo.

Wataalamu wa bustani wanashauri kwamba tuanze mwaka kwa kupanda mimea au maua ambayo hutoa oksijeni nyingi, ili pamoja na kuongeza mwonekano mzuri, itakusaidia kusafisha hewa na kuongeza mzunguko wa oksijeni itakayoongeza afya ya familia.


Ipo mimea au maua yaliyopo kwenye mazingira yetu ya kila siku, lakini tunayapuuza kwa kutojua thamani yake. Maua kama ulimi wa mama mkwe (snake plant), ua la amani (peace lily), mshubiri (aloe vera), ua buibui au lavenda na rosemary, haipaswi kukosekana nyumbani.

Wataalamu wanashauri kwamba mimea hii inafaa kupandwa ndani ili kuleta matokeo makubwa zaidi kwa kuwa uwezo wake mkubwa wa kuzalisha oksijeni hufanya hewa ndani ya nyumba kuwa safi, bora na yenye afya.

"Mimea hii huleta uzuri wa asili na pia kuboresha ubora wa hewa ambayo inawafanya wanafamilia kuondokana na msongo wa mawazo kutokana na urahisi wa ubongo kupata hewa safi muda wote. Kwa kuwa inasafisha hewa, inafanya usingizi wako uwe bora zaidi, ndio maana tunashauri ipandwe vyumbani au chooni," anasema Immaculata Mutalemwa, mtaalamu wa bustani.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
UNAJISI-KIAJE?
SIRI KALI
LONGO LONGO
'BADO'
HAIWEZEKANI KITI CHANGU CHA OFISINI KIANGUKE PEKE YAKE KAMA KIMESUKUMWA AFU'NKALIE!
SUMBA-WANGA
'MJOMBA' NISIKILIZE!
ULIANZA KAKA AFU'BA'MDOGO' BABU, NA SASA MJOMBA!
TUSIBISHANE NISHAPANDA TRENI YA UMEME LUGHA NI INGLISHI TU!
HA HA HA HAA!
ANA BAHATI HAJAKAA NA KINA NGOSHA ANGESIMULIA
UMEKAA NA WAZUNGU UME-KAUSHWA MATE KILANGA KOMO!
UMBEYA KWISHA SHUBAA MITI!
ACHA UBOYA SISI TUMEPANDA 'GOGO' TANGIA ENZI ZA MKOLONI MIMOSHI KIBAO!!!
KWA HIYO MKE ASINIPE STRESS NIJIKAZE?
UTAKUFA UTUACHIE TUMUOE!
KAJA KUPIMA NGUO AU KUNIPIMA IMANI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
HATA UMBEA NI KAZI JAPO HAUNA AJIRA...

HABARI KIMATAIFA

# Trump kusomewa hukumu kabla ya kuingia White House

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, anakabiliwa na mtihani mzito kabla ya kuingia Ikulu, kufuatia hukumu ya kesi yake kutolewa siku 10 kabla ya kuapishwa.

Jaji wa mahakama ya New York, Juan Merchan, anayesikiliza kesi ya rushwa inayomkabili anatarajiwa kutoa hukumu kabla ya kuapishwa kwake Januari 20, mwaka huu.

Jaji Merchan alisema Trump ambaye atakuwa rais wa kwanza wa zamani kuwahi kuhukumiwa kwa uhalifu, anaweza kuhudhuria kikao hicho au kupitia njia ya video.

Katika uamuzi wa awali wa kurasa 18, Merchan alikataa hoja mbalimbali za mawakili wa Trump ambao walitaka hukumu yake kutupwa.

Jaji huyo alibainisha kwamba hana nia ya kutoa adhabu ya kifungo cha jela, badala yake anaegemea katika kuachiliwa bila masharti, hukumu nyepesi ambayo hata hivyo itamfanya Trump aingie Ikulu ya White House kama mhalifu aliyepatikana na hatia.

Trump anatarajiwa kukata rufaa ambayo inaweza kuchelewesha hukumu yake.

Rais huyo mteule alipatikana na hatia katika mahakama kuu ya New York, mwezi Mei mwaka jana kwa makosa 34 ya kughushi rekodi za biashara ili kuficha malipo ya pesa alizompa nyota wa filamu za ngono Stormy Daniels kabla ya uchaguzi wa 2016.

Mawakili wake walikuwa wakitaka kesi hiyo itupwe kwa misingi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uamuzi wa kihistoria wa Mahakama ya Juu mwaka jana kwamba marais wa zamani wa Marekani wana kinga ya kutoshtakiwa kutokana na vitendo mbalimbali alivyofanya akiwa ofisini.

> **"Kesi hii ni ya uvunjaji sheria haikupaswa kamwe kuletwa na Katiba inataka itupiliwe mbali mara moja," alisema Cheung katika taarifa yake.**

Hata hivyo Jaji Merchan alikataa hoja hiyo lakini alieleza kuwa Trump hataweza kushtakiwa mara tu atakapoapishwa kama rais.

Msemaji wa Trump, Steven Cheung, alimshutumu uamuzi wa Jaji Merchan wa kutoa hukumu kwa rais huyo wa zamani na kuiita ukiukaji wa moja kwa moja wa uamuzi wa kinga ya Mahakama ya Juu na sheria zingine za muda mrefu.

"Kesi hii ni ya uvunjaji sheria haikupaswa kamwe kuletwa na Katiba inataka itupiliwe mbali mara moja," alisema Cheung katika taarifa yake.

Cheung aliongeza kuwa hakupaswa kutolewa hukumu, na Rais Trump ataendelea kupigana dhidi ya udanganyifu huo hadi utakapokoma.

Trump pia alikabiliwa na kesi mbili za shirikisho zilizoletwa na wakili maalum Jack Smith, lakini zote mbili zilitupwa chini ya sera ya muda mrefu ya kutomshtaki rais aliyekuwa mamlakani.

Katika kesi hizo, Trump alishutumiwa kwa kula njama ya kutengua matokeo ya uchaguzi wa 2020 aliyoshindwa na Joe Biden na kuondoa idadi kubwa ya nyaraka za siri baada ya kuondoka Ikulu ya Marekani.

**DW**



Raia wa Msumbiji wakikimbilia Malawi baada ya nchi yao kutawaliwa na vurugu. **PICHA: AFP**

## Waasi M23 wateka mji mwingine DRC

**GOMA,** DRC

WAASI wa M23, wanaoungwa mkono na Rwanda, wameendelea kuongeza kasi ya mapigano na kufanikiwa kuchukua udhibiti wa mji wa Katale, ambao uko magharibi mwa Goma.

Eneo hilo liko umbali wa kilomita 70 kutoka Goma ambao ni mji mkuu huo wa jimbo la Kivu Kaskazini nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Kundi la M23, waliliteka eneo la kimkakati la Katale, alasiri ya Ijumaa, baada ya mapigano makali ya siku mbili kati ya kundi la waasi hao na jeshi la DRC likishirikiana na wapiganaji wazalendo.

Kwa upande wa wanajeshi wa DRC, walisema kuanguka kwa Katale kunaleta kikwazo katika kuwarudisha nyuma waasi.

Kizuizi cha mwisho kinachoulinda mji wa Masisi ambao ni makao makuu ya utawala wa mkoa, pia inaunganisha mji wa Goma.

Katale pia inachukuliwa, kama ishara ya mafanikio ya upinzani, baada ya makundi mengi ya waasi wanaopigana mkoa wa Kivu Kaskazini hayajawahi kufanikiwa kuteka mji huo.

Ofisa wa utawala wa eneo hilo, Thierry Muhindo, alisema watu kunahama mji huo kutokana na hofu ambayo imetawala eneo hilo kutokana na kusonga mbele kwa waasi na milio ya risasi iliyosikika.

Msemaji wa wapiganaji wa Wazalendo wa eneo hilo, Kanali Séraphin Nsabimana, alihakikisha kwa upande wake kwamba kila kitu kinafanyika ili kukabiliana na kutekwa kwa mji wa Katale na waasi wa M23.

**FRI**

# Rais Korea Kusini bado ang'ang'aniwa

**SEOUL,** KOREA KUSINI

OFISI ya Uchunguzi wa Ufisadi Korea Kusini, imemtaka kaimu rais wa nchi hiyo Choi Sang-mok, kuamuru idara ya usalama kufuata agizo la kukamatwa kwa Rais aliyeondolewa madarakani Yoon Suk Yeol.

Katika tukio lilovuta hisia za watu wengi, juzi Idara ya usalama na wanajeshi, waliwazuia waendesha mashtaka kumkamata Yoon baada ya kuibuka mzozo uliodumu kwa saa sita ndani ya makazi ya rais.

Wachunguzi walipata hati ya kumkamata Yoon kutokana na kuidhinisha amri ya sheria ya kijeshi mwezi uliopita iliyodumu kwa muda mfupi.

Ofisi hiyo ya Uchunguzi wa Ufisadi kwa Maafisa wa Vyeo vya Juu, ilisema jana kwamba ilimtaka tena kaimu Rais Choi Sang-mok, ambaye ni waziri wa fedha wa taifa hilo, kuamuru idara ya usalama ya rais kuonyesha ushirikiano na kutekeleza agizo la kibali hicho.

Msemaji wa wizara ya fedha alikataa kusema chochote kuhusu ombi hilo.

Hata hivyo, Polisi walimtaka mkuu wa huduma ya usalama ya rais, Park Chong-jun, kufika kuhojiwa siku ya Jumanne, shirika la habari la Yonhap News liliripoti.

Tangazo la kutumika sheria ya kijeshi ilitolewa na Rais Yoon, Desemba 3 mwaka jana iliwashangaza Wakorea Kusini na kusababisha kutolewa kwa hati ya kwanza ya kukamatwa kwa rais huyo aliye madarakani.

**BBC**

# HABARI PICHANI




Mtambo wa ujenzi ukishindilia barabara ya muda kupisha ujenzi wa barabara ya mabasi ya mwendokasi jijini Dar es Salaam jana.



Mwendesha pikipiki ya miguu mitatu akiwa amepakia mzigo mkubwa, akipita kwenye barabara ya Morogoro eneo la Manzese, Dar es Salaam jana.



Mwananchi akichagua nguo kwa ajili ya sare ya shule eneo la Manzese, Dar es Salaam jana.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Fani Mussa, akizumgumza na wazee katika kambi ya Misufini aliowaahidi watapewa huduma ya matibabu bila malipo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Naibu Kamishina wa Ufundi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Tedy Sikiluwasha (wa pili kulia), Meneja wa Kikodi Wilaya ya Kinondoni, Azizi Rajab (kulia), wakiwakabidhi zawadi ya mlipakodi bora viongozi wa Kituo cha Sheria cha Velma Law, Habyalimana Mayeye (kushoto) na Janet Ndyetabure, jijini Dar es Salaam hivi karibuni.



Askari wa usalama barabarani akizungumza na dereva wa gari alilosimamisha katika barabara ya Morogoro, eneo la Manzese, Dar es Salaam jana.
**PICHA ZOTE JUMANNE JUMA**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-16

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WALIONEKANA kutokuwa na wasiwasi kwani mpaka muda ule hakukuwa na dalili ya polisi wala kitu chochote cha kuwatia hofu. Hata kutoonekana kwa mwenzao waliona huenda amepata tatizo la kawaida.

"Katumbukia shimoni nini maana huku kuna mashimo kweli." Alisikika mmoja. "Angepiga kelele." Mwingine aliitikia. Wakati wanabishana. Kwa kasi ya umeme, Eddy alivuka upande ule ambao walikuwa awali. Alizunguka mpaka kwenye kile kibanda. Alisubiri kwa dakika mbili, akawaona wanarejea. "Yule ameshaumwa na nyoka, ameshakufa. Kwa sababu mzigo tumeshapata na hakuna tatizo lolote hatuwezi tena kumbeba au kufanya chochote tuondokeni, kwani hili jambo tulilokuja kulifanya ni la hatari kama tukileta mbwembwe hapa tutakuja kukamatwa," aliongeza mmoja wao kwa sauti nzito akionekana kama ndiye kiongozi wa kundi.

"Dah, Pius hatunaye tena." Mmoja alidakia. "Hii inaitwa ajali kazini. Tuondokeni upesi." Akaamuru kiongozi wao. Kitu ambacho Eddy alifahamu ni kwamba hawakuja kwa daladala wala kwa miguu. Kuna sehemu ambayo watakuwa wameweka gari yao. Akaamua kuwafuata nyuma nyuma kwa uangalifu. Wala hawakwenda mbali sana. Ni kama mita 500 tu.

Ni kule ambako kuna barabara ya vumbi. Eddy alikuwa amejiandaa na awamu ya pili ya mapambano. Hii ndiyo itakuwa kubwa zaidi kuliko ile ya kumzimisha Pius kwa sumu. Kitu ambacho alikihitaji pale ni kuhakikisha hakuna yeyote atakayeondoka . Alitaka pia kuuchukua ule mkoba wa pesa wenye Shilingi milioni tano, badala ya milioni 15 urejee mikononi mwake.

Kwa hali ya kawaida haikuwa kazi rahisi hata kidogo. Waliotumwa au kujituma kuchukua hizo pesa nao walikuwa wamejidhatiti. Hawakuwa dhaifu hata kidogo kwani ni wataalamu wa hizo kazi.

Kwake Eddy alishapanga nini afanye ili alianzishe na kazi ya kupambana nao pamoja na kuurudisha mkoba mikononi mwake.

Alinyata nyuma moja kwa moja hadi alipokaribia gari lao. Ilikuwa ni Mazda CX-5 ya toleo la mwaka 2013. Alichofanya ni kuchomoa bastola yake ndogo, akalenga tairi la mbele, akafyatua risasi iliyolipasua.

Akalenga na la nyuma. Akalipasua. Hakuna aliyefahamu kwa sababu bastola aliyokuwa nayo haikutoa mlio. Ilikuwa ina kiwambo cha kuzuia sauti. Waliokuwepo ndani ya gari walikuwa bado hawajapiga stati ili gari iondoke.




**Tayari kulikuwa na watu watatu ambao walikuwa wamezirai kwa poda ya sumu. Alitoa kichupa cha dawa ya kuzuia damu akamwagia miguuni jamaa ili isiendelee kuvuja na kusababisha kupoteza maisha. Wote watatu aliwahitaji wazima.**

Walihisi gari inalalia upande mmoja wa kushoto. Haraka Eddy alizunguka upande wa pili bila kuonekana akisaidiwa na vichaka vikubwa vilivyokuwepo eneo hilo. Akafanya kama alivyofanya awali. Gari ikaonekana kushuka chini. Waliteremka wote chini ili kuangalia kuna nini.

Kila mmoja aliinama na kushuhudia pancha kwenye matairi yote manne. Wakashangaa. "Pengine tumepita sehemu yenye misumari," mmoja aliwaambia mwenzake.

Sasa aliona ni wakati wa kuwachanganya kabisa. Akachomoa ile ambayo haina kiwambo.

Akatandika risasi mbili akilenga kioo cha gari. Milio miwili ya risasi na ya kuvunjika kwa kioo kwenye eneo tulivu lililokuwa kimya eneo lile liliashiria shari. Tayari walijua hakuna usalama tena, hivyo kila mmoja aliamua kukimbia na kujitoma kwenye vichaka.

Kwa sababu hawakujua wapi zilikuwa zinatoka, mmoja tu ndiye aliyeonekana ana bastola, wengine waliobaki walionekana ni mabaunsa, mwingine akiwa amefutika bisu kubwa kiunoni.

Bahati mbaya au nzuri yule mwenye bastola alionekana kukimbilia eneo ambalo Eddy yupo.

Ni kama mnyama aliyejipeleka mwenyewe kwenye mdomo wa mamba.

Alipofika karibu na Eddy alijikuta akipigwa mtama na kukandamizwa na mguu. Wakati akitaka kupiga kelele kuita wenzake mkono wa Eddy ulikuwa umeziba puani na mdomoni. Mkono ulikuwa na unga ule ule wa sumu.

Wakati akifurukuta, ndivyo alivyokuwa akizidi kuuvuta. Ghafla nguvu zikamuishia. Akawa kama Pius. Huyu alikuwa na bastola mkononi. Hivyo ilikuwa ni faida kwa Eddy, alichukua kutoka mikononi mwake, akaifutika kwenye suruali. Mahesabu yake sasa alikuwa amebakisha watu wawili.

Kwa uzoefu wake alijua kabisa hawajaenda mbali. Alitulia kwa zaidi ya dakika 10. Kwa mbali alisikia majani makavu yakilia. Wala hakukosea. Alikuwa ni mmoja wao. Alikuwa anaondoka eneo la tukio taratibu na kwa tahadhari baada ya kujificha kwa muda.

Eddy alimuona vizuri tu. Hakutaka kujisumbua sana. Akatoa bastola yake isiyotoa sauti, akamtandika mbili za miguuni. Kelele alizopiga zilisababisha wa nne naye kutoka mafichoni na kukimbia bila mpangilio.

Nusura Eddy angue kicheko. Alinyoosha bastola yake, lakini baadaye akaghairi. "Haina maana, haina umuhimu wowote. Tayari kazi imeshamalizika," alijisemea mwenyewe. Akamwacha aondoke.

Ni mmoja tu kati ya wanne waliofika eneo lile aliyekuwa na bahati ya kuponyoka kwenye mikono ya Eddy tena kwa kutaka mwenyewe. Alijua atapatikana tu, hivyo asingeweza kumaliza nguvu kubwa au risasi bila sababu yoyote.

Alimsogelea alipokuwa ameanguka chini. Naye pia alipewa dawa ambao ilimzuia kuendelea kupiga kelele. Poda ya usingizi.

Kwenye operesheni hii Eddy hakutaka kabisa kutumia nguvu zake za sanaa ya mapigano kwani aliona ni nyepesi. Hawezi kupigana na watu wasio na uwezo wowote. Matokeo yake angewamaliza tu. Kila kitu alichokifanya kilikuwa na sababu.

Tayari kulikuwa na watu watatu ambao walikuwa wamezirai kwa poda ya sumu.

Alitoa kichupa cha dawa ya kuzuia damu akamwagia miguuni jamaa ili isiendelee kuvuja na kusababisha kupoteza maisha. Wote watatu aliwahitaji wazima. Na ndiyo maana hakuwaua, wala kuwapa majeraha makubwa kwa sababu bado alikuwa na kazi nao.

Aliingiza mfukoni na kutoa simu ya mkononi akampigia Kamanda wa Polisi Kanda Maalum.

"Habari afande." "Nzuri kijana, vipi mbona usiku huu?" "Ndiyo kamanda, ile kazi ambayo uliongea na bosi wangu nimeifanya tayari. Sasa kinachotakiwa ni kutuma askari wako maeneo ya Mikwambe hapa Kigamboni, barabara ya kutoka Kigamboni kwenda Tuangoma. Maeneo hayo kinajengwa kiwanda cha saruji.

Kuna watu watatu ambao wanatakiwa kuchukuliwa na kwenda kuhifadhiwa. Nadhani hawa ndiyo watatusaidia kufahamu kila kitu kuhusu ile inshu ya kutekwa mtoto." "Okay, wako kwenye hali gani?" "Wamezirai wote watatu, mmoja amekimbia, waliobaki wapo eneo hilo hilo, lakini sehemu tofauti. Nitakuandikia meseji ili wanaokuja wasipotee na wawapate kwa urahisi. Mimi nimemaliza naondoka, sitakuwepo tena eneo la tukio."

"Vizuri, lakini mimi nadhani suala hili ungemaliza mwenyewe, na tulichohitaji ni kukusanya ushahidi tu kwa ajili ya kuwapeleka mahakamani."

"Ni kweli kamanda, lakini bado. Suala halijaisha kabisa. Hatujajua nani yupo nyuma ya hili, mtoto hajapatikana, wala hatujui nani alikuwa anavujisha siri.

Haya mambo matatu yote ndiyo yanayotakiwa kujulikana, sijakamilisha ila niko katika hatua ya mwisho. Ila ninachoomba hao watu waweke selo, wakizinduka kesho jioni lakini msiwahoji chochote. Kuna vijana wangu nitawatuma waje kuwachukua kwa ajili

**Itaendelea Jumapili**

# MADONA UMETISHA HUYU SAWA NA MJUKUU

WAKATI vijana wa Kitanzania wanalaumiwa kwa kupenda kujihusisha kimapenzi na wanawake wenye umri mkubwa maarufu kama "Mishangazi" lakini kwa dogo mmoja imekuwa tofauti baada ya penzi lake na mwanamuziki mkongwe Madona, kumpatia umaarufu duniani.

Kijana hiyo Akeem Morris (28), alimvisha pete ya uchumba mkongwe huyo wa muziki wa Pop, Madona ambaye kwa sasa ana miaka 66.

Ukihesabu haraka Morris amepitwa miaka 32 na Madona, lakini mwenyewe anakiri kwamba haoni wala hasikii kwake kutokana na raha ya mapenzi anayopatiwa.

Katika picha zilisoambaa katika mitandao ya kijamii, Madonna anaonekana akiringa huku akionyesha kidole chake kilichong'arishwa na pete hiyo ya madini ya almasi.

Madonna aliyezaliwa Agosti 16, 1958 aliwahi kuolewa mara mbili, mara ya kwanza na mwigizaji Sean Penn kuanzia mwaka 1985 hadi 1989 na baadaye na mwongozaji wa filamu Guy Ritchie kutoka 2000 hadi 2008.

Wanaume wote waliomuoa Madona, wakikutana na Morris wanaonekana sawa na babu zake.





# ZUCHU ANAWAIMBIA WA MITAANI

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Zuchu, amesema nyimbo zake zinatokana na maisha halisi ya watu wa chini ambao hawana sehemu ya kutoa sauti zao.

Zuchu amesema hakuna nyimbo ambayo ameimba kutokana na maisha yake au kwenye mapenzi kwa sababu hayawezi kuwagusa wananchi wa kawaida.

"Nataka kutoa ujumbe wa watu wengi ambao hawana sauti hasa wanawake na watoto. Huko ndiko naungwa mkono na kupata pesa lazima niwathamini," amesema Zuchu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### REAL MADRID YAGOMEWA
LIVERPOOL imekataa mpango wa Real Madrid wa kutaka kumsajili beki wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26 mwezi huu. (**Athletic**)

### JUVENTUS YAPIGA HODI UNITED
JUVENTUS na Napoli zinania ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23. (**Mirror**)

### MAN UNITED KUUZA WACHEZAJI
KLABU ya Manchester United haina bajeti ya kuimarisha kikosi chao mwezi huu na watalazimika kuuza wachezaji kwanza kabla ya kununua ili kuendana na sheria za haki endelevu za Kifedha. (**Manchester Evening News**)

### LIVERPOOL YAPUMUA KWA VAN DJIK
WINGA wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32 na mlinzi wa Uholanzi Virgil van Dijk mwenye miaka 33, wote wanatarajiwa kuongeza muda wao wa kukaa Liverpool kwa miaka miwili. (**David Ornstein, via Mirror**)

### NUNEZ NJIANI KUPIGWA BEI
LIVERPOOL ipo tayari kumuuza mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 25, na wanamtathimini mshambuliaji wa Inter Milan na Ufaransa, Marcus Thuram mwenye umri wa miaka 27, pamoja na mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye miaka 25, kama wachezaji wanaoweza kuchukua nafasi yake. (**Teamtalk**)

### LIVERPOOL, MAN UNITED ZAGONGANA
LIVERPOOL inaweza kushindana na Manchester United katika kumuwania beki wa kushoto wa Hungary, Milos Kerkez mwenye umri wa miaka 21 kutoka Bournemouth. (**Caught Offside**)

### OLMO AZIINGIZA VITANI KLABU EPL
ARSENAL, Liverpool, Chelsea na Tottenham Hotspur zimeungana na Manchester United na Manchester City katika kuonesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Barcelona mwenye umri wa miaka 26, Dani Olmo. (**Mundo Deportivo**)

### HUIJSEN AIVUTIA REA MADRID
REAL Madrid inavutiwa na mlinzi wa Bournemouth na Hispania, Dean Huijsen mwenye umri wa miaka 19. (**Fichajes**)

### CHELSEA KUMPIGA BEI CASADEI
CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 21 ambaye ameivutia klabu ya Torino ya Italia. (**Talksport**)

### FOREST KUMPA MKATABA AINA
KLABU ya Nottingham Forest ina uhakika wa kukubaliana mkataba mpya na beki wa pembeni wa Nigeria, Ola Aina mwenye umri wa miaka 28, ambaye analengwa na Manchester City. (**Football Insider**)

### BARCELONA MACHO KWA NKUNKU
KLABU ya Barcelona sasa imeelekeza nguvu katika kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27 baada ya kuona ugumu kwa Dani Olmo.(**Offside**)

### BAYERN MUNICH YAMTAKA BART
KLABU ya Bayern Munich imeorodhesha makipa kadhaa ambao wanaweza kuwasajili msimu wa majira ya joto akiwemo mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi mwenye miaka 22, Bart Verbruggen wa Brighton. (**Bild**)

### TANGANGA NJIANI KUTUA WOLVES
WOLVES inatathmini dau la kumnunua beki wa Millwall, Japhet Tanganga mwenye umri wa miaka 25 mwezi huu. (**Express**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE BRUYNE HAKIELEWEKI MANCHESTER CITY

**MANCHESTER,** England

Kocha Guardiola ameweka wazi kuwa umri wa nyota huyo utachangia maamuzi ya....

PEP Guardiola amesema umri wa Kevin De Bruyne utachangia sana iwapo Manchester City itamuongezea mkataba mpya na kwamba klabu hiyo inabidi "ifikirie" ikiwa ni jambo sahihi kufanya hivyo.

Kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji, De Bruyne amekuwa mmoja wa wachezaji nyota wa City tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2015 lakini anafikisha umri wa miaka 34 Juni, siku chache kabla ya mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England kumalizika.

De Bruyne pia amekuwa na majeraha katika misimu miwili iliyopita na ameanza mechi nane pekee msimu huu wakati klabu na mchezaji wameshindwa kuwa na kiwango cha juu.

Amekiri kwamba mazungumzo bado hayajaanza kuhusu mkataba mpya na alipoulizwa kuhusu nafasi ya yeye kupata mkataba, Guardiola alisema Ijumaa kuwa klabu itazingatia vipengele vyote.

> **"Alikuwa na matatizo katika mwaka mmoja na nusu uliopita, kama wachezaji wengi mwaka huu," alisema bosi wa City.**

"Bila shaka, anapokuwa na msimamo na fiti na anaweza kucheza mara kwa mara, nimesema mara nyingi yeye ni mchezaji muhimu sana kwetu na mchezaji mwenye maamuzi.

"Nini kitatokea, atafanyaje hadi mwisho wa msimu, umri alionao na mambo mengine, nadhani klabu inapaswa kufikiria juu yake."

De Bruyne amehusishwa kuhamia Saudi Pro League na klabu ya MLS ya San Diego FC, na anaruhusiwa kufanya mazungumzo na klabu zisizo za Uingereza kuhusu uhamisho wa bure.

Wakati huo huo, Guardiola alisema hakujua kama itawezekana kwa City kuimarisha kikosi chao Januari.

Kocha huyo wa Hispania hapo awali alisema atakuwa tayari kutumia soko la msimu wa majira ya baridi kutafuta wachezaji, lakini alidai kabla ya pambano la Jumamosi dhidi ya West Ham United, "Sijui kwa sasa,... sio rahisi na haitakuwa rahisi.

# VINÍCIUS AOMBA RADHI KWA KADI NYEKUNDU



**MADRID,** Hispania

VINICIUS Júnior aliomba radhi baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu katika ushindi wa mabao 2-1 wa Real Madrid dhidi ya Valencia Ijumaa katika mchezo wa kwanza wa LaLiga 2025.

Hugo Duro aliifungia Valencia katika kipindi cha kwanza kwenye Uwanja wa Mestalla, huku Jude Bellingham akikosa mkwaju wa penalti na Kylian Mbappé bao lake likakataliwa kutokana na kuotea.

Vinícius alioneshwa kadi nyekundu kwa kumpiga kipa wa Valencia, Stole Dimitrievski kabla ya Luka Modric kuisawazishia Madrid dakika ya 85 na Bellingham kufunga bao la ushindi.

Matokeo hayo yanamaanisha kuwa Madrid wapo kileleni mbele ya Atlético Madrid, pointi mbili mbele ya wapinzani wao lakini wakiwa wamecheza mechi moja zaidi.

"Samahani, na asante timu," aliandika Vinícius kwenye ukurasa wake wa X baada ya mechi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alijibu kwa hasira alipooneshwa kadi nyekundu katika dakika ya 79, na akazuiwa kumkabili mwamuzi Cesar Soto Grado na mwenzake Antonio Rüdiger na kocha wa makipa Luis Llopis.

"Tunafikiri haikuwa kadi nyekundu," alisema kocha Carlo Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Timu iliweza kukabiliana na kukosa penalti na bao lililokataliwa. Ni vigumu kueleza jinsi kipindi chetu cha kwanza kilivyokuwa kibaya na jinsi kipindi cha pili kilivyokuwa kizuri... Hatuwezi kuonesha nyuso hizi mbili."

Vinicius ametolewa nje kwa kadi nyekundu mara mbili pekee akiwa na Real Madrid, huku zote mbili zikitolewa kwenye uwanja wa Mestalla.

Pia alitolewa kwa kadi nyekundu katika kipigo cha 1-0 cha Madrid dhidi ya Valencia Mei 21, 2023, mchezo ambao hapo awali alikabiliana na kundi la mashabiki wa nyumbani kwa kumzomea. "Tutakata rufaa," alisema Ancelotti.

# Mo Salah: Huu ni mwaka wangu wa mwisho

**LIVERPOOL,** England

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah amethibitisha kwamba anajiandaa kwa huu msimu wake wa mwisho katika klabu hiyo ya Merseyside huku mazungumzo yakikwama kuhusu mkataba mpya.

Mkataba uliopo wa Salah unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu huku wachezaji wenzake Trent Alexander-Arnold na Virgil van Dijk pia mikataba yao ikielekea ukingoni.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri mwenye umri wa miaka 32 hadi sasa amefurahia kampeni ya kipekee, akifunga mabao 17 na asisti 13 kwenye ligi na kuisaidia Liverpool kujikita kileleni mwa msimamo wa ligi kwa pointi sita.

Mazungumzo kuhusu mkataba mpya yamekuwa yakiendelea na kambi ya Salah kwa miezi kadhaa, hata hivyo, alithibitisha Ijumaa kuwa yeye na klabu bado wako mbali sana kufikia makubaliano.

Alipoulizwa kama anaamini huu utakuwa msimu wake wa mwisho ndani ya Liverpool, Salah aliiambia Sky Sports, "Hadi sasa? Ndiyo. Ndani ya miezi sita iliyopita, hakuna maendeleo huko, tuko mbali na maendeleo yoyote, kwa hivyo tunahitaji tu kusubiri, ngoja tuone."

Akizungumzia matamanio yake mwanzoni mwa msimu, Salah alisema: "Kitu cha kwanza ambacho kilikuwa kwenye orodha ni kushinda Ligi Kuu akiwa na Liverpool.

"Katika mahojiano yangu katika kipindi cha miaka saba au nane iliyopita, huwa nasema nataka kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini hii ni mara ya kwanza nasema nataka sana kushinda Ligi Kuu nikiwa na Liverpool."

Alipoulizwa kwa nini ni hivyo, aliongeza: "Sijui. Pengine ni kwa sababu hatukusherehekea ushindi wetu kwa jinsi tulivyotaka na pia kurudi hapa pia, ni mwaka wangu wa mwisho katika klabu hivyo unataka. kufanya kitu maalum kwa ajili ya jiji hilo ndilo jambo lililokuwa kichwani mwangu.

"Tulingojea taji hilo kwa miaka 30 au zaidi ili kulishinda na lilikuwa janga wakati huo, hatukuwa na wakati wa kusherehekea kwa njia sahihi. Sio jambo zuri kufanya, kwa hivyo. natumai tunaweza kufanya mwaka huu tena."

Mustakabali wa Alexander-Arnold ulizidi kuwa mgumu zaidi wiki hii na vyanzo vya habari viliithibitishia ESPN kwamba Liverpool ilikataa ofa kutoka kwa Real Madrid kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Uingereza.

Salah, Alexander Arnold na Van Dijk wote walipambana vizuri katika kushinda taji la Ligi Kuu kwa Liverpool katika msimu wa 2019/2020 na ushindi wao wa Ligi ya Mabingwa mnamo 2019.

Pia wameshinda Kombe la FA (2022), Carabao Cup (2022, 2024), UEFA Super Cup (2019) na Kombe la Dunia la klabu bingwa ya Dunia (2019) walipokuwa Anfield.

# Ronaldo ana njaa ya mataji

**RIYADH,** Saudi Aarabia

CRISTIANO Ronaldo ametangaza kuwa ana njaa ya kutwaa mataji zaidi katika kuadhimisha miaka miwili akiwa na klabu ya Al Nassr inayoshiriki Ligi Kuu ya Saudia Arabia.

Nahodha huyo wa Ureno, aliyetajwa kuwa Mchezaji Bora wa Mashariki ya Kati wa 2024 katika tuzo za Globe Soccer, amefunga mabao 74 katika michezo 83 tangu ajiunge nayo kwa uhamisho wa bure Januari 2023 baada ya kuondoka Manchester United.

Akitafakari enzi zake akiwa Riyadh, Ronaldo, ambaye Februari 5, anatimiza umri wa miaka 40, alikiambia kituo cha habari cha ndani cha ligi hiyo. "Nina furaha na familia yangu ina furaha. Tulianza maisha mapya katika nchi hii nzuri. Maisha ni mazuri, soka ni nzuri.

"Kwa upande wa mtu binafsi na wa pamoja, bado tupo, bado tunaboresha."

Ronaldo, ambaye amefunga zaidi ya mabao 900 katika maisha yake ya soka na kushikilia rekodi ya dunia ya wanaume kwa mabao mengi zaidi ya kimataifa, anaamini kuwa Saudia Pro League imekuwa ikisonga katika mwelekeo sahihi tangu kuwasili kwake.


"Kwangu mimi ni heshima kubwa kuwa ligi inakua na wachezaji wengi nyota wanakuja kuifanya ligi kuwa bora zaidi na yenye ushindani," alisema.

"Kuwa wa kwanza, tuseme nyota kuja hapa ni heshima, lakini ninachotarajia ni miaka mitano hadi 10 ijayo ya ligi itakuwa imeimarika zaidi, sio tu timu za kwanza, bali pia vyuo na vituo vya vijana.

"Watu wanamtazama Cristiano kama mfano, sio tu uwanjani, lakini pia nje ya uwanja."

Ronaldo ametwaa taji moja, Kombe la Klabu Bingwa Ulaya mwaka 2023, tangu ajiunge na Al Nassr.

Al Nassr wapo katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ya Saudia Pro, wakiwa nyuma kwa pointi 11 dhidi ya Al Ittihad wanaoongoza ligi.



## HABARI MICHEZO

# TABORA UNITED: CHIKOLA HAENDI KOKOTE NG'O

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United imesema kwa sasa hakuna mazungumzo na klabu yoyote yanayoendelea juu ya uhamisho wa winga wao, Offen Chikola kwa ajili ya kumsajili kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, huku ikiweka bayana kuwa haendi kokote.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Christina Mwagala amesema jana kuwa hakuna dili lolote kutoka klabu yoyote, linalomhusisha mchezaji wao huyo ambaye kwa sasa yupo kwenye majukumu na kikosi cha timu ya Tanzania Bara kinachoshiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi, Zanzibar.

Mwagala alisema hayo kufuatia baadhi ya vyombo vya habari kuripoti kuanzia juzi juu ya mchezaji huyo aliyeipa mafanikio makubwa Tabora United kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu kutakiwa na klabu ya KMC kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao.

"Kumekuwa na taarifa au tetesi za mchezaji wetu Chikola kuwa ana mazungumzo na moja ya klabu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Uongozi wetu unapenda kuwafahamisha mashabiki wa soka kuwa hakuna mazungumzo yoyote ambayo yamefanyika kati yetu na hiyo klabu kwa sababu Chikola bado ana mkataba na klabu sisi na ataendelea kuitumikia timu yetu. Kwa maana hiyo timu yoyote ambayo ingekuwa inamhitaji ingekuja kwanza kwetu, lakini pia hatuwezi kumuacha kwa sasa kwani ni mchezaji muhimu kwetu," alisema Mwagala.

Chikola amekuwa na mwanzo mzuri msimu huu akiwa na kikosi cha Tabora United ambacho kimekuwa tishio kwenye Ligi Kuu hadi kutamatika kwa mzunguko wa kwanza, ikimaliza kwenye nafasi ya tano kwenye msimamo baada ya kucheza michezo 15 na kushinda michezo saba, sare nne na kupoteza michezo minne ikiwa na pointi 25.

Wakati huo huo, klabu hiyo imesema imewapa mapumziko mafupi wachezaji wake kabla ya kurejea tena kuanza mazoezi kwa ajili ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza mwezi Machi.

Mwagala amesema mapumziko hayo yametokana na kusimama kwa ligi, lakini pamoja na hayo wameamua kutoa ya muda mfupi ili kutowafanya wachezaji wasiwe na utimamu wa mwili.

"Tumewapa mapumziko ya muda mfupi tu, nadhani mpaka mwishoni mwa mwezi huu tutarejea tena kambini kujiandaa na ligi," alisema Ofisa Habari huyo.

# KenGold yajipanga 'utukutu' wa Morrison

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa KenGold, Omari Kapilima, amesema ameandaa programu maalum kwa mchezaji Bernard Morisson, ambaye amesaini mkataba wa kuitumikia timu hiyo kwa miezi sita.

Alisema kabla ya kumsainisha walizungumza na nyota huyo na kumpa masharti ya timu hiyo ambapo ni kuona anawapa kitu cha maana ndani ya uwanja na si vinginevyo.

Kapilima alisema hayo kufuatia rekodi ya mchezaji huyo na matukio ya utovu wa nidhamu akiwa kwenye klabu za Yanga na Simba.

Kocha hiuyo alisema mbali na masharti ambayo yamo ndani ya mkataba, anadhani utukutu wake hautokuwa na athari yoyote kutokana na kuwa kwenye klabu yenye mazingira tofauti na klabu za Simba na Yanga.

"Tulishazungumza naye kumpa masharti yetu tukakubaliana naye, tunajua uwezo na uzoefu alionao utatupa kitu duru la pili kuona tunaondoka mkiani kwenye msimamo wa ligi.

Hayuko peke yake, wapo mastaa wengine kutoka Zambia na DR Congo na wengine ambao wamechezea timu kubwa hapa nchini kama Yondani, hivyo tunaenda kuanza upya ligi" alisema Kapilima.

Morrison aliyejizolea umaarufu mkubwa nchini kutokana na kipaji chake kikubwa cha soka, pamoja na aina yake ya maisha ya kujichanganya na mashabiki, aliingia nchini mwaka 2020 na kujiunga na Yanga akitokea DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, akaitumikia kwa miezi sita kabla ya kutimkia Simba alipokipiga kwa mwaka mmoja na nusu hadi 2022, aliporejea tena Yanga.

Hata hivyo hakukaa kwa muda mrefu akatimkia AS Rabat ya Morocco ambako aliitumikia kwa muda mfupi kabla ya kupata majeraha na kumaliza mkataba wa mwaka mmoja akiwa nje ya dimba.



Nyota wa Simba, Chamou Karaboue (kushoto) akichuana na Jean Charles Ahoua kwenye mazoezi ya timu hiyo jana nchini Tunisia kujiandaa na mchezo wao wa leo wa kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Sfaxien. **PICHA: SIMBA**

# Zimamoto FC kusajili watatu dirisha dogo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto SC imesema haitafanya usajili wa wachezaji wangi katika kipindi cha dirisha dogo la usajili kwa kuwa wachezaji walionao wanauwezo wa kufanya vizuri katika mzunguko wa lala salama.

Zimamoto SC ni miongoni kwa timu ambazo zimetia nia ya kuutaka ubingwa wa Ligi kuu ya Zanzibar katika msimu huu wa 2024/2025.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo Mohamed Hilali 'Tedd' alisema mapendekezo aliyowasilisha katika uongozi wa timu hiyo kuwa anahitaji wachezaji watatu ambao wataongeza nguvu timu yao.

Alisema sababu kubwa ya kusajili wachezaji hao wachache ni kutokana na kutaka kuwatumia wachezaji wao sita ambao walikuwa majeruhi na hawakuweza kutumika mzunguko wa kwanza.

Alisema wachezaji hao wote ni wakikosi cha kwanza na wana uwezo mkubwa wa kupambana na kutimiza lengo Lao.

Aidha alisema kwa wachezaji hao watatu ambao watasajiliwa ni wa nafasi mbili za washambuliaji pamoja na mlinzi wa kati ili kupata muunganiko mzuri wa kikosi cha kwanza.

"Wachezaji hawa watatu wanatutosha na tutafikia malengo yetu ambayo sisi tumejiwekea katika msimu huu ambao umeanza kwa upinzani mkali"alisema Tedd.

Hata hivyo alisema timu hiyo inatarajia kuendelea na mazoezi yake Jumatatu ya wiki hii baada ya mapumziko mafupi waliyoyatoa kwa wachezaji wao.

Zimamoto SC inashika nafasi ya tano katika msimamo wa ligi ikiwa na pointi 24 ikizidiwa pointi sita na vinara wa Ligi hiyo Mlandege FC.

# Michezo

Jumapili Januari 5, 2025
Nipashe



De Bruyne hakieleweki Man City UK. 21


# Gusa, achia yaivuruga Mazembe

## Yakumbana na kipigo cha mwaka mpya, Yanga yaweka hai matumaini ya...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikiwa inahitaji pointi tatu muhimu kuweka hai matumaini yao ya kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga jana iliisambazia 'Gusa, achia, twende kwao' TP Mazembe na kuifumua mabao 3-1 kwenye mchezo uliochezwa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ushindi huo sasa umeifanya Yanga kufikisha pointi nne na kupanda mpaka nafasi ya tatu kwenye msimamo wa kundi A na kuiacha TP Mazembe ikiburuza mkia kwa pointi zake mbili huku Al Hilal ikiongoza kundi kwa pointi tisa na kufuatiwa na MC Alger wenye pointi nne sawa na Yanga lakini leo watakabiliana na vinara kwenye mchezo mwingine wa kundi hilo.



Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kushoto) akiwatoka mabeki wa TP Mazembe kwenye mchezo wa hatua ya Makundi Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa jana uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Yanga ilishinda 3-1. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

Katika mchezo wa jana uliokuwa na mvuto, mabao mawili ya Clement Mzize na kiungo mshambuliaji Stephan Aziz Ki yalitosha kufifisha matumaini ya Mazembe kucheza hatua ya robo fainali.

Matokeo ya jana yalikuwa kama marudio ya kile kilichotokea, Februari 19, 2023, Yanga ilipoifunga timu hiyo idadi kama hiyo ya mabao kwenye uwanja huo huo katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Jana TP Mazembe ndio walikuwa wa kwanza kupata bao katika dakika ya 15 lililofungwa kwa mkwaju wa penalti na golikipa wake Aliou Badara Fatty.

Kipa huyo raia wa Senegal, aliamua kwenda mwenyewe kupachika mpira wavuni, baada ya kutokea adhabu hiyo kubwa iliyotokana na Shadrack Boka, kumkwatua beki wa kulia wa Mazembe, Ibrahim Keita ndani ya eneo la hatari.

Bao hilo lilionekana kuwaamsha Yanga, ambao waliamua kuliandama kama nyuki lango la wapinzani wao, huku wakikosa mabao ya wazi kila wanapofika langoni.

Dakika ya 20, wachezaji wa Yanga waligongeana mpira vizuri lakini mpira wa mwisho ulimkuta Aziz Ki, lakini alipiga nje.

Alikuwa Mzize aliyewainua vitini mashabiki wa Yanga baada ya kupachika bao la kusawazisha dakika ya 32 kwa shuti kali la mbali.

Baada ya TP Mazembe kufanya shambulizi, Yanga ilijibu kwa kuanzisha mpira haraka na kupasiana kwa haraka kabla ya mpira kumfikia Mzize aliyeachia shuti kali la juu, mpira ukamshinda kipa, Fatty na kujaa wavuni.

Kipindi cha kwanza kama Yanga ingekuwa makini ingeweza kupata walau mabao manne, kwani baada ya kufungwa bao hilo, wachezaji wa TP Mazembe walionekana kuchanganyikiwa na kutoa mianya kwa wapinzani wao ambao walifanya mashambulizi ya hatari, dakika ya 34 na 37 kupitia kwa Aziz Ki na Pacome, lakini hawakuwa makini kukwamisha mipira wavuni.

Hatimaye, Aziz Ki, alisawazisha makosa yake ya kukosa mabao mara kwa mara alipopachika bao maridadi dakika ya 56, kwa kumpiga tobo kipa Fatty.

Boaz Ngalamulume alirudisha mpira nyuma ambao ulinaswa na wachezaji wa Yanga na kupasiwa Khalid Aucho aliyempenyezea Aziz Ki ambaye alimfunga kwa tobo Fatty na kuiandikia Yanga bao la pili.

Dakika tatu baadaye, Mzize kwa mara nyingine alifunga bao lingine, likiwa la tatu kwa Yanga baada ya kuwazidi mbio mabeki wa TP Mazembe kabla ya kubaki na kipa na kuupeleka mpira upande wa kushoto wa golikipa na mpira kujaa nyavuni.

Kipigo hicho rasmi kimefuta matumaini ya TP Mazembe kutinga hatua ya robo fainali msimu huu kwani nayo ilikuwa ikihitaji ushindi kufufua matumaini yao.

# Fadlu: CS Sfaxien hawachomoki leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Simba, leo itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi, nchini Tunisia kucheza mchezo wa raundi ya nne hatua ya makundi dhidi ya, CS Sfaxien, huku Kocha Mkuu, Fadlu Davids akisema kutokana na mazoezi, mbinu na maelekezo aliyoyatoa kwa wachezaji wake, anaamini watapata ushindi kwenye mchezo huo.

Akizungumza akiwa mjini Tunis, Fadlu, alisema baada ya kuwaangalia wapinzani wake jinsi wanavyocheza, amewapa wachezaji wake mbinu za kucheza nao, akiwaelekeza wachezaji jinsi gani wanatakiwa kucheza wakati wakiwa na mpira na vipi wazuie wakati wakiwa hawana mpira miguuni.

Fadlu alisema amewakumbusha wachezaji wake kuwa makini na makosa madogo madogo ambayo yalifanyika kwenye mchezo dhidi ya CS Constantine nchini Algeria na kusababisha kupoteza kwa mabao 2-1.

"Maandalizi ya mechi yamekamilika, kilichobaki ni kwenda kutimiza kile nilichowaambia wachezaji uwanjani, kila mmoja anatakiwa atimize majukumu yake. Tumeiangalia timu hii udhaifu wake na nguvu zake, nimewapa wachezaji wangu mbinu za kuwakabili, nadhani hawatoniangusha.

Nimewaambia wasirudie tena makosa yaliyofanyika kwenye mchezo dhidi ya CS Constantine, kwani makosa binafsi yaliathiri mchezo mzima tukajikuta tunapoteza katika mechi ambayo ilibidi tuondoke na pointi tatu au moja," alisema kocha huyo.

Mchezaji mwandamizi wa timu hiyo, Shomari Kapombe, amesema yeye na baadhi ya wachezaji wenzake hawana wasiwasi kwani wameshacheza sana na timu za Afrika Kaskazini maarufu kama timu za 'Waarabu', hivyo wanajua jinsi gani ya kuwakabili.

"Sisi kama wachezaji tumeshacheza sana na Waarabu, kuna aina fulani ya uchezaji wao wakiwa nyumbani, huwa wanafanya mashambulizi makali mwanzoni ili kupata mabao ya mapema, lakini nina imani kwa mbinu anazotupa mwalimu na anazoendelea kuelekeza hadi tutakapoingia uwanjani, tutajua jinsi gani ya kuwadhibiti," alisema Kapombe.

Nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala', amesema kitu ambacho wanaingia kupigania katika mchezo wa leo ni ushindi ili kurahisisha kazi ya kutinga hatua ya robo fainali kwani kwa misimu yote wamekuwa wakifika hatua hiyo baada ya michezo ya mwisho.

"Safari hii wachezaji tumeambizana tufuzu robo fainali mapema tofauti na misimu iliyopita na ili iwe hivyo ni lazima tushinde mchezo huu," alisema.

Simba ambayo ipo kwenye Kundi A, inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo ikiwa na pointi sita, iwapo itashinda leo itafikisha pointi tisa huku ikiwa imebakisha michezo miwili dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola ugenini na CS Constantine nyumbani.

Wenyeji wa mchezo huo, CS Sfaxien wanakwenda kucheza mechi ya nne ikiwa haina pointi yoyote katika michezo mitatu iliyocheza mpaka sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >